# Uhuru na Amani

GAZETI LA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA TOLEO LA 2, 2016 Bei Sh. 1,000/-



## YALIYOMO NDANI:


- Vijana msitumike kisiasa
- Toleo maalumu la Vijana ndani
- Umoja usiwe wa kinadharia
- Utatu Mtakatifu: Ni Mungu 3?
- Kanisa la Msumbiji laimarika
- Fahamu tunu za KKKT?
- Tuwekeze kwa vijana wetu
- KCMC kutibu kansa Septemba


Vol. 116, Toleo la 2, 2016 ISSN 0856 - 1214

# FAHAMU TUNU ZINAZOONGOZA KKKT

Na Mallumbo W. Mallumbo



**Mallumbo W. Mallumbo,**
**Naibu Katibu Mkuu Mipango na Maendeleo, KKKT.**

## UTANGULIZI

Kadri tulivyojifunza historia ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kama ilivyoainishwa katika Toleo la Kwanza la Gazeti hili la 'Uhuru na Amani' mwaka 2016 (Vol. 116, Toleo la 1, 2016); Kanisa limeendelea kukua na kumhudumia mtu kwa ukamilifu - kiroho, kiakili na kimwili kama ilivyonenwa na kuelekezwa na kiongozi wetu, yaani Yesu Kristo. Bwana Yesu anasema katika Maandiko Matakatifu (Biblia): ***"Roho wa Bwana yu juu yangu; Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru walioteswa, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa",*** (Lk. 4: 18-19). Japo umaskini unaozungumzwa ni wa moyo, vivyo hivyo ulikuwa ni wa kipato kwa sababu wenye mali na madaraka hawakuwa na nafasi ya kumsikiliza Bwana Yesu wala manabii waliomtangulia. Watu walifungwa na minyororo ya umaskini na maradhi. Ujinga ulitawala na Bwana Yesu aliweka mfano wa kuigwa alipotangaza vita dhidi ya tamaa ya mali, maradhi, umaskini na ujinga. Haya ndiyo mambo yanayoonekana katika tangazo lake hilo. Na kwa ajili hiyo Kanisa linatoa huduma za kijamii sambamba na kufanya kazi ya kueneza huduma ya kiroho ili kuenenda na utume huu.

Pamoja na Matengenezo ya Kanisa yaliyofanyika kupitia muasisi wake Mchg. Dkt. Martin Luther; KKKT inaongozwa na Taswira (maono), Dhamira na Tunu ambavyo ni vitu vya msingi katika kuonesha uhalisia wa uwepo wake, utofauti wake na wengine, nk.

Tunu za KKKT ni pamoja na:

## MAISHA YA USHUHUDA

Kanisa linasisitiza kuwa kila Mkristo aishi maisha yenye kukiri na kutangaza matendo makuu ya Bwana wetu Yesu Kristo.

## UWAZI

Vitabu vya mahesabu ya KKKT hukaguliwa na wakaguzi wa ndani na wa nje. Hii ni kuonesha kwamba mali na fedha ni mali za wakristo wenyewe na siyo mali ya mtu binafsi au viongozi. Kila juma Washarika hupewa taarifa ya makusanyo ya sadaka /mapato yote na taarifa ya robo mwaka hutolewa kwa washarika ili wafahamu mwenendo wa mapato na matumizi. Hivyo mwenye mamlaka na mali za Kanisa ni mkristo na huu ndio uwakili mwema.

## UWAJIBIKAJI

Kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu, watumishi na wakristo wanatambua wajibu na majukumu yao na hufundishwa umuhimu wa kuwajibika ili kutomlemea mtu yeyote kama anavyotuongoza Mtume Paulo (2The 3: 6-8). Mkazo wa Kanisa katika utumishi, kazi na maisha ni kuwa na bidii, ubunifu na weledi. Kutowajibika au kutokufanya kazi kwa bidii humfanya mtu kuwa maskini wa kipato bali afanyaye kazi kwa bidii huneemeshwa (Mithali 28:19).

## UTETEZI

Miongoni mwa mataifa na hata ndani ya Kanisa yapo makundi yaliyosahauliwa kama wanawake, watoto, wazee, wenye magonjwa ya muda mrefu, wenye ulemavu, nk. Jamii imeyasahau na hata kupora haki zao za msingi. Watoto wenye ulemavu wameonekana kama laana na hivyo kufungiwa ndani, kukosa elimu na huduma za afya, nk. Wanawake wananyimwa haki ya kumiliki ardhi na hata kushika nafasi ya kuongoza jamii kwa sababu ya mila potofu. Watu wenye ulemavu wamenyimwa haki ya kupata elimu, ajira na mikopo na hakuna wa kuwatetea. Ndio sababu Kanisa linasimama na kupaza sauti kwa niaba yao au kwa kupitia wao. Kanisa linawasemea wanyonge kwa kuhusika kikamilifu katika harakati na kuishawishi Serikali na wenye mamlaka kuboresha/ kuisimamia Sera na Mikataba ya Taifa/ Kimataifa inayolinda/ kutetea haki za binadamu.

## CHACHU YA MAENDELEO

Tunashukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweka mazingira mazuri kwa Kanisa kufanya shughuli mbalimbali nchini. Serikali yetu imetoa uhuru na mwanya ambao haupo katika baadhi ya nchi barani Afrika. Kutokana na fursa hiyo KKKT imekuwa chachu njema katika kuchangia maendeleo ya nchi. Kwa mfano baada ya Serikali kuruhusu uanzishwaji wa vyuo vikuu huria nchini Chuo Kikuu cha Tumaini kilikuwa cha kwanza kuanzishwa na madhehebu ya dini nchini na KKKT ni taasisi ya kidini ya kwanza kuanzisha Benki ya Uchumi (Dayosisi ya Kaskazini).

Tunamshukuru Mungu kwa kuliwezesha Kanisa kutoa huduma za afya kuanzia zahanati, vituo vya afya hadi hospitali za rufaa kama vile hospitali ya Haydom (Mbulu) na KCMC (Moshi) ambazo ni hospitali za rufaa. Kanisa lilianzisha Shirika la Kimisioni la Kusambaza Madawa na Vifaa Tiba (MEMS) linalohudumia hospitali mbalimbali nchini na hivyo kuipunguzia mzigo Bohari ya Taifa ya Madawa (MSD). MEMS kwa sasa inaendeshwa kwa pamoja na Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) na Kanisa Katoliki kupitia Kamisheni ya Huduma za Kijamii ya Kikristo.

Yalipojitokeza maafa na majanga kama ukame, mafuriko, magonjwa ya milipuko au wimbi la wakimbizi; Kanisa halikunyamaza ila lilitoa huduma kwa uhusiano wa karibu na Ofisi ya Waziri Mkuu. Hospitali ya Kilutheri ya Selian (Arusha) ni taasisi ya kwanza nchini kuanzisha Huduma ya Tiba Shufaa (Palliative Care). Na miaka ya hivi karibuni, Kanisa kwa mara ya kwanza limeziwezesha Hospitali za Kanisa na baadhi ya hospitali za Serikali kuunganishwa katika mfumo wa kompyuta wa ukusanyaji, utunzaji na utoaji taarifa za wagonjwa kwa kupitia programu iitwayo 'Care2X' iliyobuniwa na Kitengo cha Teknolojia ya Habari cha KKKT. Baadhi ya hospitali za Serikali zilizonufaika na programu hiyo ni Hospitali ya Rufaa Mbeya, Hospitali ya Mirembe na Kibong'oto. Si muda mrefu, Kanisa linatarajia kutibu magonjwa ya Kansa katika hospitali ya KCMC, Moshi na hivyo kuipunguzia mzigo Hospitali pekee ya Taifa ya Kansa (Ocean Road Cancer Institute) iliyopo Dar es Salaam. Lengo ni kupunguza idadi ya vifo, hasa vya watoto wa Kitanzania, vinavyo sababishwa na ugonjwa huo. Mungu mwenyewe anayawezesha haya yote kwa kuwatumia watu wake wakiwemo watumishi, viongozi wa Kanisa, washirika wa ndani na nje waliojitoa na kuchangia kwa hali na mali kwa ajili ya ustawi wa watu wengine.

## KUTANGAZA WOKOVU

Tangu wakati wa Dkt. Martin Luther, Kanisa limeendelea kuwahubiria watu ***Habari Njema*** yaani Injili ya kumjua, kumpokea na kumuishia Bwana Yesu Kristo. Kanisa haliendekezi mila na tamaduni za watu au jamii fulani na wala halipo kwa ajili ya kutoa hukumu bali kufundisha, kutangaza neema, msamaha na kuwawezesha watu kumjua Mungu wa kweli aonekanaye kupitia Yesu Kristo mfufuka ambaye kwa kadri ya Maandiko Matakatifu na imani yetu, atarudi tena katika hali ya utukufu wa Mungu Baba.

## MSAMAHA NI KWA NEEMA NA IMANI KWA YESU KRISTO

Msamaha hupatikana kwa njia ya toba ifunikwayo na neema ya Mungu mwenyewe kupitia Yesu Kristo. Wokovu haupatikani kwa nguvu ya kiuchumi au nafasi katika jamii bali ni neema tu ituokoayo. Twahubiri na kusisitiza kuwa kusamehe na kusahau ndiyo siri ya kusamehewa. Ndiyo maana Sala Kuu husema: ***"Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni, utupe leo riziki zetu, utusamehe deni zetu kama sisi nasi tunavyo wasamehe waliotukosea. Usitutie majaribuni; bali utuokoe na yule mwovu; kwa kuwa wako ni ufalme, nguvu na utukufu; hata milele na milele,"*** (Mt. 6:9b-13).

**Uhuru na Amani**
Gazeti la KKKT
**Toleo la 2, 2016**
Vol. 116 Na. 2
**ISSN 0856 - 1214**

Uhuru na Amani ni Gazeti la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hutayarishwa na Kitengo cha Mawasiliano, KKKT.
Maoni yaliyomo katika makala zinazochapishwa ni ya mwandishi anayehusika na wala hayawakilishi mawazo ya Kanisa ama mhariri isipokuwa pale ambapo imetamkwa wazi.
Ukiwa na maoni, ushauri, makala au maswali mwandikie:
**Mhariri**
**Uhuru na Amani**
**S.L.P. 3033**
**ARUSHA**
**Barua pepe:** elobulu@elct.or.tz
**Sms** Whats App kwa Mhariri: +255-754-482-285
**Fungua Tovuti ya KKKT:** http://www.elct.org/

**MHARIRI**
**Elizabeth Lobulu**

Limepigwa Chapa na:
**Moshi Lutheran Printing Press**
S.l.P 301 Moshi
Moshilutheranpress@gmail.com

Newspaper Design & Typesetting:
**Elizabeth Lobulu**

**Wachangiaji wa Makala:**
Askofu Amon Mwenda
Mwl. Tumaini Chambua
Mallumbo W. Mallumbo
Mchg. Anza Amen Lema
Dkt. Zebadia Mmbando
Mchg. Lazaro Rohho
**Wachangiaji Picha:**
Mchg. Anza Amen Lema
Mchg. Lazaro Rohho
Mchg. Katri Kuusikallio, FELM

**PICHA YA JALADA:**
Mkuu wa KKKT akifurahia jambo huku amezungukwa na baadhi ya vijana waliohudhuria Kongamano la Nne la Vijana KKKT lililofanyika 4 - 8 Juni mwaka huu. Kongamano hilo lililohudhuriwa na vijana 700 lilifanyika Shule ya Msingi ya Martin Luther, Dodoma.

# MAONI YA MHARIRI

## Tuuishi umoja wetu

Akifungua Kikao cha Halmashauri Kuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kilichofanyika Moshi tarehe 21 - 22 Aprili 2016; Mkuu wa Kanisa, Askofu Dkt. Fredrick Shoo, aliwataka viongozi wa Kanisa watunze umoja wa Kanisa kwa vitendo kwa kutimiza wajibu wa Kikatiba, kutekeleza maamuzi ya pamoja na maongozi yanayowekwa na Mkutano Mkuu.

Aliwasihi wajumbe wapatao 70 toka Dayosisi za KKKT wathamini dhamana kubwa waliyopewa na Mungu ya kutunza msingi wa imani na kusudi la Kanisa kwa kujitoa kwa dhati na kwa moyo na kwa kujiweka chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu.

Alisema: "Kila mmoja na wote kwa pamoja wakati wote tunapaswa kujiuliza ni nini Bwana wa Kanisa anachotaka kwa Kanisa lake kwa wakati huu? Tunachangiaje katika kuyatimiza mapenzi ya Bwana wa Kanisa kwa Kanisa lake katika nafasi zetu?

"Maswali hayo si jambo la maneno tu bali ni jambo la matendo, si jambo la kiakili tu bali hasa ni jambo la kiroho. Akinukuu toka Biblia alisoma: 'Si ninyi mlionichagua mimi bali mimi ndiye niliyewachagua ninyi, na nikawaweka ili mpate kunizalia matunda, na matunda yenu yapate kukaa ili kwamba lolote mmwombalo Baba kwa jina langu awapeni,' (Yohana 15: 16).

"Kutokana na wito wa kumzalia Bwana matunda yanayokaa inatulazimu kuacha ubinafsi kwa kufikiri kupita mipaka ya umimi tu, au kipindi changu tu, au dayosisi yangu tu au kizazi chetu tu kwa kukubali kuwa tumeitwa na tumewekwa ili tuzae matunda yatakayoendelea kuwepo hata baada yetu.

"Waasisi wa Kanisa la KKKT toka makanisa saba yaliyoungana na kuanzisha KKKT waliongozwa na roho ya kuzaa matunda yanayokaa. Waasisi hao walitambua tunda la kwanza na muhimu sana ni 'umoja' jambo ambalo waliliainisha vizuri katika Katiba" alisema na kuongeza kuwa viongozi waliopo sasa wanapaswa kuiendeleza roho ya umoja kwa 'kuuhifadhi na kuukuza umoja wetu,' (Efeso 4: 3).


Mkuu wa Kanisa alisema umoja wo wote unadai kuwajibika kwa kweli; kuaminiana na kuwa na uwazi. Hivyo viongozi wajitoe kuimarisha umoja wa Kanisa letu kwa kutekeleza yale wanayo kubaliana kikatiba. "Sio kujiuliza napata nini kwanza bali ni kujiuliza nachangia nini?" Alifafanua.

Pili alitaka viongozi watambue kwamba umoja una gharama zake, hivyo wanapaswa kujiuliza wanawajibika kiasi gani kuuimarisha na kuuendeleza umoja wa Kanisa.

Alisema kwa kuwa umoja wa kanisa ni kwa ajili ya waumini wote wake kwa wanaume, watoto kwa vijana, walei kwa Wachungaji, makabila na maeneo tofauti kijiografia; hivyo ni muhimu kuimarisha roho ya uongozi bora kwa kutekeleza mipango ya kuwaendeleza watu.

Alisema "tujiulize tunaimarishaje roho ya kuaminiana, kushauriana na kutunzana kwa uwazi na upendo. KKKT ni Kanisa kubwa miongoni mwa Makanisa ya Kilutheri Duniani na akalifananisha na mnyama mkubwa ambaye alisema anatakiwa kuzinduka na kudhihirisha kwa vitendo uwepo wake. "Na tukimtegemea Bwana na kutaka kweli kuujenga umoja tutafanikiwa," Mkuu wa KKKT alisema.

# Wachungaji 2,000 wa KKKT kukutana Dodoma 2016





Askofu Dkt. Abednego Keshomshahara wa Dayosisi ya Kaskazini Magharibi (katikati) atafundisha mada kuhusu Miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa. Anaonekana pichani akiwa na Askofu Amon Kinyunyu wa Dayosisi ya Dodoma (kulia) na Askofu Dkt. Alex Mkumbo wa Dayosisi ya Kati wakiwa Halmashauri Kuu ya KKKT iliyokutana hivi karibuni.

Katibu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Bw. Brighton Killewa pichani kulia, ametangaza hivi karibuni kwamba Mkutano wa Wachungaji wote wa KKKT unatarajiwa kufanyika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) 24 - 29 Septemba. Watakao hudhuria ni wajumbe wapatao 2000 kutoka Dayosisi zote, Maeneo ya Misioni ya KKKT na Vituo ya Kazi za Umoja. Mada zitakazotolewa zinalenga kujenga na kuimarisha Umoja wa Kanisa kama sehemu ya maadhimisho ya ***"Miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa"*** chini ya kichwa ***"Ushuhuda wetu".*** Mada ni kama ifuatavyo: "***Elimu ya Kikristo"; "Kanisa na Uamsho"; "Ushauri Kichungaji"*** na ***"Ibada na Umoja wa Kanisa".***

Mara ya mwisho mkutano wa Wachungaji wote wa KKKT ulifanyika Chuoni UDOM mwaka 2010.

Akizindua kamati ya maandalizi kwa ajili ya tukio hilo mnamo Juni 20, Bw. Killewa aliomba Washarika waombee mkutano huo na aliwataka wajumbe wafanye maandalizi kwa bidii na uaminifu ili Mkutano wa Wachungaji uwe wa mafanikio. Aliwaambia: ***"Mwenende kama wito wenu mlioitiwa kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo; na kujitahidi kuuhifadhi umoja katika kifungo cha amani,*** " (Efeso 4: 1-4).

# Mkutano Makanisa ya Tanzania na Ujerumani



Ujumbe wa watu saba toka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ulioongozwa na Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo, ulialikwa na uongozi wa Muungano wa Makanisa ya Kilutheri Ujerumani (VELKD), Ujerumani 4 - 10 Machi 2016. Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa kikao kama hicho kuhudhuriwa na Mkuu wa KKKT awamu ya tano.

Kwenye ziara hiyo Mkuu aliongozana na Mkuu wa KKKT aliyemaliza muda wake KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, ambaye pia ni Makamu wa Rais Kanda ya Afrika wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) aliyefuatana na Mchg. Dkt. Elieshi Mungure, Katibu wa Afrika FMKD.


Washiriki wengine walitoka Sweden na Finland. Pamoja na mambo mengine washiriki walihudhuria semina na kufanya ziara maeneo mbalimbali kama mji wa Wittenberg na kutembelea Ofisi ya "Bread for the World" na jiji la Berlin.

# Viongozi wa KKKT na CSSC wakutana



Viongozi wa Kamisheni ya Huduma za Jamii ya Jumuiya a Kikristo Tanzania (CSSC) hivi karibuni walikutana na viongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kuhusu kuhamishwa kwa shughuli za Shirika la Misioni la Madawa na Vifaa Tiba (MEMS) kutoka KKKT kwenda CSSC. Hii ni kutokana na patano la Halmashauri Kuu ya KKKT kwamba MEMS iunde kampuni na hivyo shughuli zake zihamie CSSC Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa aliongoza timu ya menejimenti ya Kanisa na Mkurugenzi Mtendaji wa CSSC Bw. Peter Maduki alifuatana na Dkt. Josephine Balati, Mkurugenzi wa Afya, CSSC.

# Mwakilishi wa vijana Marekani afika



Mwakilishi wa Vijana toka Kanisa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani (ELCA), Mchg. Louis Tillman alitembelea Ofisi Kuu ya KKKT baada ya kushiriki katika Kongamano la Nne la Vijana KKKT lililofanyika Dodoma Juni 4 - 7 mwaka huu. Mchg. Tillman alilishukuru Kanisa kwa kumkaribisha na alisema amejifunza mambo mengi toka Tanzania. Mchg. Lazaro Rohho, NKM Misioni na Uinjilisti (kushoto) akimtambulisha Bw. Tillman kwa watumishi wa Ofisi Kuu ya Kanisa.

# Mkuu ataka vijana wasitumiwe kisiasa

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dkt. Fredrick Shoo, alikifungua Kongamano la Nne la Vijana wa KKKT lililofanyika katika Shule ya Msingi ya Martin Luther, Dodoma 4 - 8 Juni 2016 alionya watu waache kutumia matatizo ya vijana kwa kuwatumia katika makundi ya kisiasa.


Alisema kwa kukosa fursa ya ajira na namna ya kuwapa kipato cha uhakika baadhi ya wanasiasa walio wabinafsi hudanganya na kuwatumia vijana kutekeleza agenda za kisiasa.

Mratibu wa Vijana KKKT, Mchg. Anza Amen Lema, alisema Kongamano hilo lililohudhuriwa na washiriki 700 toka Dayosisi za KKKT na maeneo ya Misioni lilifanya harambee kwa ajili ya kununua shamba la kupanda miti kama kitega uchumi cha kusaidia kutoa huduma za vijana wa KKKT siku zijazo. Mkuu aliongoza Ibada ya ufunguzi kwa kushirikiana na Askofu Kinyunyu ambaye alifunga Kongamano kwa kuongoza Ibada ya Chakula cha Bwana. Neno Kuu la Kongamano lilikuwa: "Tupate wapi mtu kama huyu, mwenye roho ya Mungu ndani yake?" (Mwa. 41: 38b) lililoongozwa na Mchg. Dkt. George Mark Fihavango, Msaidizi wa Askofu wa Dayosisi ya Kusini. Vijana 700 walishiriki katika Kongamano hilo.



**Mkuu wa Kanisa, Askofu Dkt. Fredrick Shoo (aliye na fimbo mkononi), katika picha ya pamoja baada ya kufungua Kongamano la Nne la Vijana KKKT 2016. Kutoka kulia ni Mmiliki na ambaye pia ni Mkurugenzi wa Shule ya Martin Luther, Bw. Abel Mmanga. Kulia kwa Mkuu ni mkewe, Mama Janet Shoo; akifuatiwa na Askofu Amon Kinyunyu, Mkuu wa Dayosisi ya Dodoma. Wengine ni Mchg. Anza Amen Lema, Mratibu wa Vijana KKKT; Mchg. Louis Tillman, Mwakilishi wa Vijana kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani na Bw. Shemeji Melayeki, Mwezeshaji wa Mada kutoka Dayosisi ya Kaskazini Kati.**

# Papa Francis kushiriki kumbukumbu ya Matengenezo ya Kanisa



**Papa Francis,
Kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani.**



**Mchg. Dkt. Martin Junge, Katibu Mkuu wa FMKD.**



**Askofu Dkt. Munib A. Younan, Rais wa Fungamano la Makanisa la Kilutheri Duniani.**

Papa Francis, Rais wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), Askofu Dkt. Munib A. Younan, na Katibu Mkuu wa FMKD, Mchg. Dkt. Martin Junge, watashiriki Ibada ya pamoja 31 Oktoba mwaka huu kuadhimisha Siku ya Matengeneo ya Kanisa.

Tukio hilo la kihistoria litafanyika mjini Lund, Sweden kama sehemu ya maandalizi ya kumbukumbu ya miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa 2017. Pia itakuwa ni kumbukumbu ya miaka 50 ya majadiliano baina na Kanisa la Kilutheri na Kanisa Katoliki yenye lengo la kuondoa uhasama na kujenga umoja wa Kanisa ulio wito wa Kristo.

Kwa taarifa kutoka Fungamano hilo, Mchg. Dkt. Junge alisema hivi karibuni "ipo nguvu pale jamii zinapotafuta suluhu ya migongano maana katika Kristo tumetumwa kuhudumu duniani kwa kushirikiana." Naye Mhashamu Kadinali Kurt Koch, Rais wa Baraza la Kipapa la Kukuza Umoja wa Kikristo alisema: "kwa kuwa mjadala umelenga kutazama masuala kuhusu Mungu na mtazamo kuhusu Kristo; Walutheri na Wakatoliki watafanya kumbukumbu ya Matengenezo ya Kanisa kiekumene na kwa dhati kwa kuwa sote tunamwamini Yesu aliyesulubiwa na kufufuka." Watu wapatao 10,000 wanatarajiwa kushiriki katika matukio hayo.

Ibada itafanyika Kanisa Kuu la Lund na baadaye kutakuwa na matukio na maelezo zaidi jijini Malmö katika uwanja ujulikanao kama Malmö Arena. Askofu Mkuu wa Kanisa la Sweden, Antje Jackélen, alisema kwamba lengo ni kueleza zaidi kuhusu matumaini ya siku zijazo na maeneo zaidi ya kushirikiana katika kutoa huduma duniani baina ya makanisa hayo mawili.

Askofu Anders Arborelius wa Dayosisi ya Kanisa Katoliki Stockholm alisema, "Historia itaandikwa kwa viongozi hao kukutana ili kututia moyo wa kuendeleza safari ya umoja wa Kanisa la Kikristo".

## NI JUNGE TENA FMKD

Mkutano wa Halmashauri Kuu ya FMKD iliyokutana katika mji wa Kihistoria wa Lutherstadt Wittenberg, Ujerumani hivi karibuni ilimteua Dkt. Junge kuwa Katibu wa Fungamano hilo kwa kipindi cha pili. Uteuzi huo unaanza Novemba Mosi 2017 hadi 2024. **(Chanzo: LWI/ FMKD)**

# Hospitali ya Kanisa kutibu kansa

Hospitali ya Rufaa ya Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC) iliyopo Moshi ambayo inasimamiwa na Shirika la Msamaria Mwema imeanza ujenzi wa kituo cha kutibu ugonjwa wa kansa. Hayo yalisemwa na Kaimu Mkurugenzi wa Afya na Diakonia wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dkt. Zebadia Mmbando, hivi karibuni aliporejea toka Marekani kwa mwaliko wa Taasisi iitwayo Foundation for Cancer Care in Tanzania (FCCT) ya Minnesota, Marekani ambayo ni washirika wa huduma ya afya KKKT na kujionea jitihada za uchangiaji wa fedha kwa ajili ya kituo hicho.

Kituo hicho kinachojengwa na Kanisa, hospitali ya KCMC, na kwa ushirikiano na FCCT ulianza mwanzoni mwa mwaka huu na awamu ya kwanza itakamilika Septemba. Alisema tiba ya Kansa kwa watoto itaanza kutolewa Septemba mwaka huu. FCCT ni wahisani wakubwa wa ujenzi, ununuzi wa vifaa tiba, samani na madawa.

Katika awamu ya pili FCCT itagharamia ujenzi wa hosteli ya watoto na wazazi/walezi wao wakati wakisubiri tiba. Hatua hiyo itafuatiwa na ujenzi wa jengo pamoja na miundo mbinu kwa ajili ya kutibu kansa kwa watu wazima. Hii ni pamoja na uwekaji wa mashine inayotumia teknolojia ya kisasa ya tiba ya mionzi iitwayo “Linear Accelerator” au “LINAC radiation Machine.” Dkt. Mmbando aliomba wote tumshukuru Mungu anayawezesha haya yote kwa kuwatumia watu wake wakiwemo watumishi, viongozi wa Kanisa, washirika wa ndani na nje waliojitoa na kuchangia kwa hali na mali kwa ajili ya ustawi wa watu wengine. Huduma hiyo ikianza KCMC, itapunguza mzigo wa Hospitali ya Taifa ya Kansa ya Ocean Road iliyopo Dar es Salaam. Alisema mazungumzo yanaendelea ili kushirikiana na kupata utaalamu katika tiba shufaa na tiba ya kansa KCMC na katika hospitali za KKKT zinazotoa huduma ya tiba shufaa.



**Dkt. Zebadia Mmbando, Kaimu Mkurugenzi wa Afya na Diakonia, KKKT (kulia) akimtambulisha Dkt. Reena George toka Hospitali ya CMC Vallore, India (kushoto) na Mchg. John Lunn, Mratibu wa Global Health Volunteers ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani walipotembelea Ofisi Kuu ya KKKT hivi karibuni ili kuendeleza mazungumzo kuhusu Huduma za Tiba Shufaa na Kansa zinazotolewa na Hospitali za Kanisa.**

# Selian yaongoza kwa huduma ya fistula nchini

Katibu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Bw. Brighton Killewa, 26 Mei 2016 alikabidhi Gari aina ya LandCruizer kwa Hospitali ya Kilutheri ya Selian iliyopo Ngaramtoni, Arusha ili kutumika kutoa huduma ya tiba ya fistula iliyoanzishwa na hospitali hiyo tangu 2001. Katika hafla fupi ya makabidhiano hayo katika Ofisi Kuu ya KKKT, Katibu Mkuu alisema Kanisa linatimiza wito mkuu wa kuhubiri Injili kwa ukamilifu kwa kumhudumia mwanadamu kiakili, kimwili na kiroho ndiyo sababu linatoa huduma mbalimbali za kijamii ikiwa ni pamoja na huduma za afya.

Mkugurugenzi wa Hospitali ya Kilutheri Selian, Dkt. Amon Israel Marti, alisema huduma ya fistula ilianza 2001 baada ya madaktari bingwa wawili wa upasuaji kupata mafunzo yao nchini Ethiopia ambapo wagonjwa 20 hadi 40 walipasuliwa kwa mwaka. Mwaka 2011 daktari bingwa wa upasuaji wa fistula kutoka Australia alijiunga na timu ya Selian na ikaonekana kuna umuhimu wa kuwa na kliniki nje ya kituo (outreach clinic) ili kueneza habari za fistula na kuibua wagonjwa walio majumbani waweze kupata huduma. Awali walikuwa wanatumia gari la Hospitali ambalo ni chakavu na huduma yao imefika Mikoa tisa yaani Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro, Dodoma, Singida, Shinyanga, Mwanza na Tabora. Hata hivyo wamewahi kupokea wagonjwa toka Rukwa na Kagera. Dkt. Marti alisema Selian kimekuwa miongoni mwa vituo vikubwa vya upasuaji wa fistula barani Afrika kwani kutokana na kufanya safari hizo za kuibua wagonjwa katika mikoa hiyo kwa sasa Hospitali ya Selian inauwezo wa kupasua wagonjwa




180 wa fistula kwa mwaka. Wagonjwa wote wanaofika hospitali Selian wanapatiwa matibabu ya fistula bure ambapo matibabu hayo hulipiwa na Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania (CCBRT) na Taasisi ya Tanzania iitwayo Maternity Africa inayopata uhisani wa Taasisi iitwayo Barbara May Foundation ya Australia. Wakati wa makabidhiano Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini Kati, Bw. Samwel Njake ole Saiguran alikuwa amefuatana na Katibu Mkuu Msaidizi wa Dayosisi hiyo, Mchg. Jasson Kahembe na Katibu wa Afya wa Dayosisi, Dkt. Simon Megiroo. Bw. Saigurani alitumia fursa hiyo kushukuru Kanisa kwa kuona umuhimu wa huduma hiyo ambayo ameahidi itatumika kufanya kazi iliyokusudiwa kwa kuweza kuwafikia watu wengi zaidi wanaoteseka kwa kukosa matibabu ya fistula.

# Makanisa 3 Namibia yaandaa Mkutano Mkuu wa FMKD

**Waziri wa Kuondoa Umaskini na Ustawi wa Jamii nchini Namibia, Askofu Mstaafu Dkt. Zephania Kameeta, ambaye pia ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), Juni 2 aliwasha taa kuashiria kuanza rasmi kwa maandalizi ya mwaka mzima ya Mkutano Mkuu wa 12 wa Fungamano hilo utakafanyika jijini Windhoek, Namibia tarehe 10 - 16 Mei mwakani. Namibia ina makanisa matatu ya Kilutheri.**

**Takriban watu 500 walihudhuria Ibada na sherehe hizo zilizofanywa katika viwanja vya Bunge la nchi hiyo. Miongoni mwa wageni mashuhuri waliokuwepo ni pamoja na Dkt. Nickey Iyambo, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Namibia na Rais wa FMKD Askofu Dkt. Munib A. Younan.**



# Umoja wa Kanisa usiwe kinadharia - Askofu

Na Askofu Amon Mwenda, KKKT Dayosisi ya Ruvuma (DARU).



Askofu Amon Mwenda, KKKT Dayosisi ya Ruvuma (DARU) kushoto akifuatiwa na Askofu Ambele Mwaipopo wa Dayosisi ya Ziwa Tanganyika, Askofu Job Mbwilo wa Dayosisi ya Kusini Magharibi, Askofu Japhet Mengele wa Dayosisi ya Kusini na Askofu Sanga wa Dayosisi ya Kusini Kati wakiwa katika Halmashauri Kuu ya KKKT.

Kwa kurejea hotuba ya Mkuu wa Kanisa wa Awamu ya Tano, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, alipofungua Halmashauri Kuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) tarehe 25 Aprili 2016, mjini Moshi kwa maoni yangu "Umoja wa KKKT" unatakiwa uimarike kama agizo la Bwana wetu Yesu Kristo alivyotaka na kuagiza.

KKKT tunashirikiana vizuri katika matukio ya Kikanisa. Inabidi sasa tupige hatua kwa umoja huo kuonekana zaidi katika maisha ya kila siku ya Kanisa. Isiwe kwamba kila mmoja yuko kwake na mahusiano ya kawaida yasiwepo.

Umoja aliougaiza Bwana Yesu ulilenga mahusiano ya karibu kama jamii na kila mmoja kuwa na wajibu wa kujua na kumtambua mwenzake na kushirikiana naye katika changamoto zinazomkabili. Neno linasema kila mmoja ni kiungo kwa mwenzake.

Umoja wa KKKT umejengwa juu ya msingi wa Yesu Kristo, Inafaa basi kuendelea kuukuza katika msingi huo hasa kwa sasa wakati ambapo Kanisa limekuwa na kupanuka sana.

Kwa pamoja tuhakikishe hakuna tofauti kubwa mno ndani yetu kati ya Dayosisi changa na zile zilizo imara ili umoja uwe wa dhati na si umoja wa nadharia.

Katika Hotuba yake Mkuu wa KKKT alisema "tunahitaji kuwa na umoja wa vitendo" ili kuenzi, kulinda msingi uliowekwa na waasisi wetu. Tunahitaji kuwa na maono ya umoja kwa upya, na hapa kuna haja yakuangalia mfumo uliopo unavyotuweka pamoja; pia tuzipitie Katiba za Dayosisi na mapokeo yetu.

Mataifa makubwa na yaliyo endelea yanazungumza kuungana yaani umoja, ili kuongeza nguvu zao kukua kiuchumi. Kama Kanisa lenye jukumu la kumhudumia mwanadamu kimwili, kiroho na kiakili; kukidhi mahitaji haya na umoja wake ukashuhudiwa pande zote; linahitaji mshikamano toka kwa kila mmoja wetu, kuanzia aliye juu sana mpaka wa mwisho.

Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeheshimu na kuenzi mawazo au dhamira ya waasisi wetu.

Licha ya kutofautiana kiuchumi, kimaadili na tamaduni za maeneo yetu lakini utambulisho wetu kihuduma kutoka nyanja nilizozitaja hapo nyuma tunakaribia sana.

Ili pawe na umoja zaidi kivitendo ni wakati muafaka KKKT kupanuka katika mipango yake ya kimaendeleo kwa kuwa na huduma za kijamii au vitega uchumi kwenye Dayosisi zake zote kutokana na fursa zinazojitokeza sasa na ukubwa wa Kanisa.

Zitakapojitokeza fursa za ajira (hasa katika vituo vya Kazi za Umoja) na upana wa Kanisa ukazingatiwa; hatua hiyo itakuwa ni mojawapo ya alama za umoja wa kweli kivitendo, (Zab. 133:1).

# Umoja upo tangu Kanisa la Mwanzo

Na Mwl. Tumaini Chambua

**UTANGULIZI**

Unapo zungumzia umoja wa Kanisa hapa duniani huna budi kuangalia asili ya umoja wa Kanisa. Umoja huu ulianza katika Kanisa la kwanza baada ya Pentekoste. Ukisoma Mdo. 2:44 na kuendelea unapata ujumbe ufuatao: ***"Umoja wa Kanisa umejengwa katika Ushirika na Upendano ambao msingi wake ni imani kwa Yesu mfufuka."*** Mambo yote katika kanisa la kwanza yalifanywa kwa ushirika na upendo, hapakuwa na tofauti yoyote kati ya waumini katika maisha yao ya kiroho hata ya kimwili.



Mwl. Tumaini Chambua, Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Pare (kulia) akifuatiwa na Mkuu wa Kanisa aliyemaliza muda wake, Askofu Dkt. Alex Malasusa, na Bw. F. Nyamoga Katibu Mkuu Dayosisi ya Ziwa Tanganyika walipokuwa katika kikao cha hivi karibuni cha Halmashauri Kuu ya KKKT.

**UMOJA WA KKKT**

Umoja wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanganyika/ au Tanzania (KKKT) unatokana na tamko la kuunganisha makanisa saba ya Kilutheri mwaka 1963. Makanisa hayo ni: Kanisa la Kiinjili la Tanganyika ya Kaskazini Magharibi; Kanisa la Iraqw; Tanganyika ya Kaskazini; Tanganyika ya Kati; Ubena - Konde; Usambara - Digo na Uzaramo - Uluguru.

Kanisa limekuwa na kuenea karibu maeneo yote ya Tanzania; bado Kanisa limeendelea kuwa moja lenye Dayosisi zinazo shirikiana katika mambo yanayoziweka pamoja licha ya tofauti za kimazingira na desturi. Kanisa limejishughulisha sana na umoja kwa kuendesha shughuli nyingi za umoja kama mikutano, vituo vya umoja, miradi ya Kanisa zima na uendeshaji wa Ofisi Kuu. Umoja wa Kanisa unaonekana katika utendaji wake. Pamoja na utendaji, Ibada za Kilutheri zinaonyesha umoja na utambulisho wetu Walutheri. Vipo vitabu vinavyotumika kwa sharika zote za KKKT ambavyo vinaelekeza utaratibu wa Ibada. Ni muhimu kuenzi umoja huu. Neno la Mungu linasema: ***"Tazama jinsi ilivyo vema na kupendeza, Ndugu wakae pamoja, kwa umoja,"*** (Zab 133:1). Watu wanaweza kuwa pamoja lakini hawana umoja, kila mtu anafanya tofauti na mwingine hata kama wameweka utaratibu wa kukaa mahali pamoja.

Makanisa yale saba yaliona umuhimu wa umoja tangu 1946 yalipounda Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Tanganyika lakini yakaona kuna umuhimu wa kuwa na kanisa moja ndipo mwaka 1963 yakaungana. Kwa kuzingatia mabadiliko ya sasa ya kiuchumi, nguvu ya umoja inahitajika kwa kiwango kikubwa ukilinganisha na mwaka 1963. Nguvu ya Kanisa itaonekana pale wanakanisa watakapoamua kwa dhati kuwa na **umoja wa kweli.** Katika kuimarisha umoja Kanisa linayo '**Siku ya KKKT'** inayokumbukwa mwezi Juni kila mwaka. Siku hii ni muhimu na sadaka ni moja inayotolewa kwa kazi za Kanisa. Inapotolewa na kuwasilishwa kwa uaminifu, inadhihirisha umoja wa kweli ndani ya Kanisa. Nguvu sahihi ya umoja wa KKKT inaonekana katika utoaji wetu kwa mambo yanayo tuunganisha pamoja.

# Mkuu ataka watumishi wa Kanisa wafanye kazi kwa moyo



Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo, akiwa katika picha ya pamoja na viongozi /watumishi wa Ofisi Kuu ya KKKT, iliyopo Arusha. Alipokutana na watumishi wa Kanisa kwa mara ya kwanza baada ya kuingizwa kazini kuwa Mkuu wa KKKT Awamu ya Tano, Dkt. Shoo aliwataka watumishi wa Kanisa kufanya kazi kwa moyo na kukubali kuongozwa na Roho Mtakatifu ili kumzalia Bwana matunda yanayodumu na si kutegemea tu uwezo wao wa kibinadamu.

## Chuo Kikuu cha Tumaini chadahili zaidi ya 10,000

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA) Profesa Joseph Parsalaw aliiambia Halmashauri Kuu iliyokutana Moshi hivi karibuni kwamba TUMA na vyuo vikuu vishiriki hadi Aprili 2016 vilikuwa kimedahili wanafunzi 10,502 kwa mwaka wa masomo 2015/ 2016 na kuhitimisha jumla ya wanafunzi 4,131 katika fani mbalimbali 2014/ 2015.



Profesa Joseph Parsalaw akitoa taarifa wakati wa Halmashauri Kuu ya KKKT.

## Kanisa la Sweden lateua Mwakilishi mpya



Bw. Leonard Forslund, Katibu wa Afrika Mashariki katika Kanisa la Sweden (katikati), alitembelea Ofisi Kuu ya KKKT na Ofisi ya LMC hivi karibuni. Mwakilishi huyo anachukua nafasi iliyoachwa na Bw. Lennart Adreasson aliyestaafu mwishoni mwa mwaka jana. Kulia ni Bw. M. Mallumbo, Naibu Katibu Mkuu Mipango na Maendeleo KKKT na kushoto ni Bi Eva Palmqvist, Afisa Uhusiano wa Kanisa la Sweden nchini.

## Dayosisi 2 zazidi kung'ara 10 bora KKKT

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) lina shule 66 za Sekondari zilizofanya mtihani wa Kidato cha Nne 2015. Shule kumi bora KKKT zilipewa tuzo na Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo, hivi karibuni. Orodha ni kama ifuatavyo: Dayosisi ya Kusini shule zilizoshinda ni Kidugala Lutheran Junior Seminary (LJS), Mufindi Girls Lutheran Secondary School (LSS) na Igumbilo LSS; Dayosisi ya Kaskazini shule zilizoshinda ni Agape LJS, Masama Girls SS na Boloti LSS. Shule nyingine katika orodha hiyo ni Shule ya Sekondari LJS Morogoro (KZU); Ailanga LJS (Dayosisi ya Meru); Bukoba LSS (Dayosisi ya Kaskazini Magharibi) na Karagwe SS (Dayosisi ya Karagwe).



Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Fredrick Skoo akimpongeza Askofu Isaya Japhet Mengele (kulia) kwa kuwa Dayosisi ya Kusini ilitoa shule 3 kati ya shule 10 bora za KKKT zilizohitimisha wanafunzi wa Kidato cha Nne 2015.



Msaidizi wa Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, Mchungaji Elingaya Saria alipokea tuzo kwa niaba ya shule 3 za Dayosisi zilizoshinda 2015.

# TOLEO MAALUMU:
# KONGAMANO LA 4 LA VIJANA KKKT

**NENO KUU: “Tupate wapi mtu kama huyu, mwenye roho ya Mungu ndani yake?” (Mwa. 41: 38b)**



Kutoka kulia ni Mchg. Ridson Kaaya toka Dayosisi ya Meru, Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Fredrick Shoo, Mchg. Mathayo Mtui toka Dayosisi ya Kaskazini, Askofu Kinyunyu wa Dayosisi ya Dodoma, Mchungaji Dkt. George M. Fihavango, Mwandishi wa Kitabu, Mchg. Lazaro Rohho, NKM Misioni na Uinjilisti KKKT na Mchg. Anza Amen Lema, Mratibu wa Vijana KKKT. Mchg. Kaaya na Mchg. Mtui walimzawadia Mkuu nakala ya kitabu kilichowekwa kwenye mnada.

## Vijana msibweteke mtiini Mungu na kufanya bidii

Na Mchg. Dkt. George M. Fihavango

Vijana msibweteke bali ishi kwa kutii na kutekeleza Neno la Mungu na kufanya kazi kwa bidii. Wale walioajiriwa wajihusishe na ujasiriamali mdogo mdogo ili kuingiza kipato cha ziada kwa maendeleo ya familia.

Mfano wa Yusufu katika Kitabu cha Mwanzo 41: 38b unafundisha kwamba kijana anapaswa kukimbia uovu au dhambi jambo linaloonesha heshima na utii kwa Mungu licha ya mazingira ya utandawazi na vishawishi yanayotuzunguka.

Mtu mwema hata akiingia matatani kama ilivyokuwa kwa Yusufu alipochukiwa na ndugu zake na kuuzwa utumwani Misri (Mwa 37: 12 - 27). Alipotupwa gerezani kwa kukataa kishawishi cha mke wa Potifa (Mwa 39: 7 - 20) lakini baraka za Mungu zilimiminika kwake popote alipokuwa. Akiwa gerezani alikuwa na bidii ndipo akawekwa kusimamia wafungwa wengine (Mwa 39: 21- 23). Alitafsiri ndoto ya mnyweshaji wa mfalme na baada ya miaka miwili yule mnweshaji alimkumbuka ndipo akatolewa jela ili atafsiri ndoto ya mfalme (Mwa 41: 14 - 36). Kwa bidii yake na kwa kuwa pia alikuwa akiongozwa na Roho wa Mungu Yusufu alipata sifa za kumfanya awe “Waziri Mkuu” ugenini Misri. Baada ya kupokea tafsiri ya ndoto na ushauri wake na kukubaliana nao, mfalme alisema ***“Tupate wapi mtu kama huyu mwenye roho ya Mungu ndani yake?”*** (Mwa 41: 38b). Mfalme aliona Yusufu ndio mtu huyo. Kijana unapaswa kujitambua na kudhihirisha ulivyo mahiri, mwenye bidii, mwadilifu na unaye Roho wa Mungu ndani yako ili na wanadamu waweze kukuchagua kuongoza.



Vijana wakisubiri ufunguzi wa Kongamano lao. Washiriki 700 waliweza kuhudhuria Kongamano la vijana 2016.



Kwaya ya Dayosisi ya Dodoma iliyonyakua ushindi wakati wa Tamasha la Uimbaji.

Kijana usikubali kupoteza muda kusoma/ kuangalia na kusambaza taarifa /picha zisizo na faida kwenye kompyuta au mitandao ya kijamii kama ‘Facebook’, ‘WhatsApp’, ‘Instagram’ au ‘Tweeter’. Ingefaa vijana mkitumia huduma hizo kwa maendeleo ya kijamii na ya familia yako.

**Mawasiliano na Mchg. Dkt. George Fihavango tuma sms 0756 761 903.**

# Kijana Mkristo anapaswa kujitambua

**Wakati wa Kongamano la Nne la Vijana KKKT Mada kuhusu Kijana Mkristo na Kujitambua na Kijana Mkristo na Matumizi ya Mitandao ya Kijamii kwa Faida ziliongozwa na Bw. Shemeji Melayeki toka Dayosisi ya Kaskazini Kati. Fuatili alichosema:**

Nashauri vijana mjitambue kwanza maana msipojitambua, hakuna atakayewatambua. Hivyo vijana watumie vipawa vyao kuigusa jamii. ***"Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi,"*** (1 Timotheo 4:12).

Kuna mifano ipatayo 58 katika Biblia ya watu maarufu wakiwemo wazee saba na vijana 51. Tukumbuke kwamba maisha ya ujana ni zama za nguvu na ujanani ni kilele cha nguvu.

Kama tusomavyo kwamba fahari (glory) ya vijana ni nguvu zao, na uzuri wa wazee ni kichwa chenye mvi (Mithali 20: 29).

Tunaambiwa "Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako, Kabla hazijaja siku zilizo mbaya, Wala haijakaribia miaka utakaposema, Mimi sina furaha katika hiyo. (Mhubiri 12:1)


Tusipoteze muda, raslimali na nguvu bali tuielekeze kwenye manufaa kwa kufanya kazi kwa bidii bila kuchoka.

"Haya vijana watazimia na kuchoka, na wanaume vijana wataanguka; bali wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka, watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia, (Isaya 40:30-31).



**Bw. Shemeji Melayeki. Yeye ni Mjasiriamali, Mshauri/ mhamasishaji na mwandishi wa vitabu. Anapatikana kwa sms: +255 763 965 297**


# Kitabu chapigwa mnada kuchangia mradi



**Mchg. Dkt. George M. Fihavango, Msaidizi wa Askofu wa Dayosisi ya Kusini aliyetoa hotuba ya Neno Kuu katika Kongamano la Vijana 2016.**



**Bw. Ebenezer Shayo, Mwenyekiti wa Vijana KKKT, alisoma Risala kwa niaba ya washiriki wa Kongamano.**



**Mchg. Lewis John Hiza toka Dayosisi ya Mashariki na Pwani alifundisha mada kuhusu "Kijana Mkristo na Maadili".**

Wakati wa Kongamano la 4 la Vijana Mkuu wa Kanisa, Askofu Dkt. Fredrick Shoo, alizindua kitabu: ***"Tumpate Wapi Kijana Kama Huyu"*** kilichoandikwa na Mchg. Dkt. George Mark Fihavango, Msaidizi wa Askofu Dayosisi ya Kusini.

Kitabu hicho ni maalumu kwa ajili ya Kongamano la Vijana 2016.

Baada ya kuzinduliwa na Mkuu, kitabu kilinunuliwa na wajumbe ndani na nje ya ukumbi wa mkutano. Kongamano lililohudhuriwa na vijana 700 lilifanyika katika Shule ya Msingi ya Martin Luther mjini Dodoma. Mchg. Ridson Kaaya toka Dayosisi ya Meru na Mchg. Mathayo Mtui toka Dayosisi ya Kaskazini walimzawadia Mkuu wa Kanisa nakala ya kitabu hicho kilipopigwa mnada.

Mratibu wa Vijana KKKT, Mchg. Anza Amen Lema alisema lengo la harambee ni kutafuta fedha za kuanzisha Mradi wa Vijana wa KKKT kwa kununua shamba na kupanda miti. Shamba la ekari 1,000 limepatikana Mkoani Katavi katika Dayosisi ya Ziwa Tanganyika.

Alisema kutokana na uwekezaji katika shamba hilo fedha zitakazo patikana zitatumika kuendesha kazi za vijana katika Kanisa.

Katika harambee hiyo kiasi cha sh. 1,900,000 kilikusanywa ukumbini hapo na ahadi ilikuwa sh. 500,000/-.



**Vijana walipata fursa ya kutembelea kiwanja cha watoto Shule ya Martin Luther.**




**Mwl. Anania A. Kelakela kutoka Dayosisi ya Mashariki na Pwani aliwezesha mada kuhusu Uimbaji Sanifu na pichani anaonekana akitathmini Kwaya wakati wa "Tamasha la Uimbaji".**



Vijana walihamasishana kushindana kuchangia mradi wa miti Kidayosisi.

# Vijana tumieni nguvu na maarifa kunufaisha Kanisa na jamii



Mchg. Anza Amen Lema, Mratibu wa Vijana KKKT.

Kijana anapaswa na ingefaa sana atumie vipawa alivyonavyo kwa kufanya kazi kwa ustadi kwa sifa na utukufu wa Mungu. Na wakati wote afikiri namna gani ataweza kufanya mambo ya kusaidia jamii.

Kijana anapaswa kuwa mfano wa kuigwa kwa walio rika lake hata kama hawana upeo kama wake na aweze kuigwa na walio wadogo.

Hivyo kwa kuwa kijana huangaliwa na wengine inabidi sasa ajipambanue kwa kuacha kufanya yale ambayo ni chukizo kwa Mungu wala asiwe kero kwa jirani. Kwa mfano kwa sasa katika jamii ya Tanzania kuna vijana wengi ambao wamesababisha nguvu kazi kupotea kwa sababu ya ulevi wa pombe na madawa ya kulevya. Vijana mnaombwa kuzingatia maonyo kuhusu ulevi mliyopata wakati wa mafundisho yenu katika mafundisho ya Kipaimara, Umoja wa Vijana na hata katika mahubiri ya kila Jumapili; katika semina za Neno la Mungu na mikutano ya Injili.


Kuanzia mavazi na tabia lazima zioneshe mwelekeo wake wa maisha na si kupeperushwa na mafundisho potofu toka kwa utamaduni wa kigeni kupitia intaneti au mitandao ya kijamii.

Kijana atumie nguvu zake za ujana vizuri kwa kuelekeza katika maendeleo ya kiakili, kiroho na kimwili ili jamii nayo iweze kuwa na mabadiliko.

Kuwa na malengo kwamba baada ya muda fulani uwe umefikia ndoto yako na kujiandaa kwa hali yo yote ile ili ndoto yako isikatizwe kwa kukata tamaa au kupotezwa na watu wasio na nia njema kwako.

Na katika maono au ndoto zake kijana anapaswa kuwa na ndoto ya kuisaidia jamii. Kwa mfano endapo ataanzisha ujasiriamali mdogo kwa ajili ya kuongeza kipato chake itasaidia kuongeza ajira katika jamii.

Umoja iwe ndio nguzo ya kijana tangu katika ngazi ya kifamilia hadi katika jamii. Hivyo kijana anatarajiwa kujihusisha na majukumu ya kifamilia na ya kijamii.





Vijana wa Dayosisi ya Kaskazini Mashariki wakishiriki Tamasha la Uimbaji.



Kwaya na vikundi vya Dayosisi vikishiriki Tamasha la Uimbaji.

# Programu za vijana zipewe rasilimali

Mwenyekiti wa Vijana, KKKT Bw. Ebenezer Shayo akisoma Risala ya Vijana kwa Mkuu wa Kanisa alipofungua Kongamano la Nne la Vijana lililofanyika mjini Dodoma 4 – 7 Juni aliahidi vijana kuendelea kuwa na umoja kama Bwana Yesu livyoagiza kwamba "Wote wawe na umoja..." (Yn 17: 21).

Alisema zaidi ya asilimia sitini (60%) ya idadi ya watu nchini ni vijana na watoto. Na robo ya washarika wote ni vijana (miaka 15 – 35) hivyo ni muhimu kuwa na mipango kwa ajili yao kwa kutumia karama zao kwa ufanisi.

Alitoa rai kwamba Dayosisi na maeneo ya Misioni KKKT yatenge raslimali kwa ajili ya kuendeleza programu za vijana na kuwashirikisha katika maamuzi na huduma mbalimbali za Kanisa.

Alisema Kanisa limeshuhudia baraka kubwa ya vijana wenye vipawa/ karama ila kilichobakia ni kuona jinsi gani vipawa hivyo vitatumika kwa ufanisi hasa kwa kuwezeshwa na kuelekezwa ipasavyo, alifafanua.

Kitengo cha Vijana, pamoja na majukumu mengine, kinaratibisha shughuli za vijana katika Kanisa kikishirikiana kwa karibu sana na viongozi wa vijana toka Dayosisi na Maeneo ya Misioni. "Hivyo katika kujenga umoja wa vijana ambao ndio Kanisa la sasa na la baadaye; tunahitaji uvumilivu na nia ya dhati ya kuwashirikisha vijana katika mipango na huduma mbalimbali za Kanisa, alisema na kuongeza kuwa vijana wamefanikiwa msaada wa Mungu, kuandaa makongamano manne: la kwanza lilifanyika Dayosisi ya Morogoro 2009; la pili Dayosisi ya Iringa 2011; la tatu Dayosisi ya Meru 2013. Na la nne ni Dayosisi ya Dodoma 2016.

Lengo kuu la Kongamano ni kuwapa fursa vijana ili kujengana kiroho na kudumisha umoja wa Kanisa letu kwa njia ya mafunzo, kushirikishana vipawa na karama mbalimbali.

Kongamano lilienda sambamba na Tamasha la Uimbaji ambalo lilihusisha Dayosisi, Maeneo ya Misioni ambapo Kwaya ya Dayosisi ya Dodoma iliibuka mshindi.

Bw. Shayo alieleza kuwa uongozi wa vijana kupitia Halmashauri yake huaandaa maadhimisho ya Juma la Vijana ambalo lilianza kuadhimishwa mwaka 2013 baada ya kupitishwa na Halmashauri Kuu ya Kanisa.



Mchg. Mimii Brown toka Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria akimsalimu Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo huku Mwenyekiti wa Vijana KKKT, Bw. Ebenezer Shao (nyuma) anayetoka Dayosisi ya Kaskazini akifurahia jambo fulani. Mchungaji Mimii Brown aliwapima vijana Ufahamu wao wa Biblia.

Katika Sharika vijana hukutana ili kushirikishana vipawa na karama zao kwa kufanya maombi, kutafakari Neno la Mungu, kufanya uinjilisti wa nyumba kwa nyumba, kutembelea/ kuombea wagonjwa, yatima, wajane pamoja na watu wenye kuhitaji faraja.

Vijana wanafanya kazi za mikono, usafi wa maeneo ya Kanisa na kuongoza Ibada ya Jumapili katika Juma la vijana huambatana na sadaka maalumu ya huduma ya vijana kwa ngazi zote.

Mafanikio mengine ni kufanyika kwa Mikutano Mikuu ya Vijana. Mkutano Mkuu wa kwanza wa Vijana uliofanyika 2012 ambao pamoja na mambo mengine ulichagua wajumbe wa Halmashauri ya kwanza ya Vijana. Mkutano wa pili ulifanyika 2014. Mipango inafanywa Mkutano Mkuu wa Tatu ufanyike mwaka huu 2016.

Kusudi kubwa la Umoja wa Vijana wa Kanisa letu ni kuendelea kuwaunganisha vijana katika Kanisa kumjua Yesu Kristo, Mwokozi wetu. Vijana wanahimizwa washiriki katika huduma na majukumu ya Kanisa kwa njia mbalimbali wakitumia vipawa na karama walizopewa na Mungu.

Mwenyekiti huyo alisema Kitengo cha Vijana kina changamoto za ukosefu wa raslimali muhimu kwa maendeleo ya kazi za vijana.



Askofu Amon Kinyunyu wa Dayosisi ya Dodoma alifunga Kongamano kwa kuongoza Ibada ya Ushirka Mtakatifu.



Vijana wakishiriki Kongamano.

# Mkuu alishukuru Kanisa kwa kuwa na imani naye

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) alitumia nafasi ya kufungua kikao cha Halmashuri Kuu ya KKKT kilichokutana Mwezi Aprili, kulishukuru Kanisa na hasa wajumbe wa Halmashauri Kuu kwa kupendekeza majina ya Maafisa wa Kanisa na wajumbe wa kamati mbalimbali na bodi za Kanisa na hatimaye kuchaguliwa kwake na Mkutano Mkuu wa 19 wa KKKT Agosti 2015.

Kipekee alimshukuru Askofu Dkt. Alex Malasusa, Mkuu wa Kanisa aliyemaliza muda wake kwa uongozi wake. Askofu Dkt. Malasusa ni Mkuu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani na Makamu wa Rais wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (Kanda ya Afrika).

Wakati huo huo takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Katibu Mkuu hivi karibuni zinaonesha kuwa Kanisa lina Wachungaji 2,209; Wainjilisti 6,413 na Wakristo karibu milioni saba. Pia ziko Sharika za KKKT 1,279; majimbo 131; Nyumba za Ibada 5,126 na mitaa 5,979. Huu ni ukuaji ambao unaambatana na changamoto mbali mbali za kiuchumi, kijamii na kiroho.



Wajumbe wa Halmashauri Kuu kutoka kushoto Bibi Mary Laiser, Mwenyekiti Halmashauri ya Wanawake KKKT, akifuatiwa na Bibi Jane Mkimbo, Katibu Mkuu Dayosisi ya Kusini Mashariki na Bibi Loe-Rose Mbise, Katibu Mkuu Dayosisi ya Meru.

# Kanisa la Kilutheri Msumbiji laimarika

Na Mchg. Lazaro Rohho, Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti, KKKT.



NKM Misioni na Uinjilisti KKKT, Mchg. Lazaro Rohho (aliye na vitabu) na uongozi uliochaguliwa hivi karibuni kuongoza Kanisa la Msumbiji. Wa tatu kulia ni Mchg. Eduardo Sinalo aliyechaguliwa kuwa Askofu na Mkuu aliyemaliza muda wake Askofu Jose Mabasso yuko kulia.

Amani imerejea katika Kanisa la Kilutheri Msumbiji baada ya Mkutano Mkuu wa Kanisa hilo kukutana mwezi Mei katika hali ya amani na kufanya uchaguzi.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na wadau wengine ni wajumbe wa Bodi ya Misioni ya Kanisa la Msumbiji (Joint Mission Board).

Amani ilitoweka katika Kanisa hilo wakati wa Mkutano Mkuu uliofanyika mjini Gorongosa, Msumbiji Novemba 2015 pale ambapo Askofu Jose Mabasso alikwazwa na hoja za wajumbe na kuondoka wakati mkutano ukiwa unaendelea. Hali hiyo ilisababisha wajumbe kwa kauli moja kumchagua Mchg. Abel Macuacua kuwa Askofu, jambo ambalo halikukubaliwa na Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Kanda ya Kusini mwa Afrika (LUCSA).

Kwa mujibu wa Katiba ya Kanisa hilo, Askofu siyo Mwenyekiti bali Mwenyekiti ni Mkristo raia anayechaguliwa na Mkutano Mkuu.

Jambo hilo lilizungumzwa tena wakati wa kikao cha pamoja cha Bodi ya Misioni ambayo inaundwa na walezi wa Kanisa hilo ikiwa na wajumbe toka KKKT, LUCSA, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani (ELCA), Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Kusini mwa Afrika (ELCSA) na Kanisa la Kilutheri Brazil. Bodi hiyo iliazimia kuwa Mkutano Mkuu maalum uitishwe ukiwa na agenda mbili ambazo ni: Kufanya marekebisho ya Katiba na kufanya uchaguzi wa viongozi wa Kanisa hilo.

Jitihada za walezi hao zilizaa matunda mema baada ya maafikiano katika Kanisa la Msumbiji kufikiwa kwa kuitishwa Mkutano Maalum uliofanyika Mei 13 - 15, 2016 katika Kituo cha Mikutano cha Nasa mjini Nampula.

Mkutano huo ulifanya marekebisho muhimu ya Katiba na hatimaye kufanya uchaguzi wa viongozi wakuu pamoja na wajumbe wa Halmashauri Kuu.

Viongozi waliochaguliwa ni Mwenyekiti Bibi Fransisca Diego aliyechaguliwa tena; Katibu Mkuu mpya aliyechaguliwa ni Mchg. Abel Macuacua na aliyechaguliwa nafasi ya Askofu ni Mchg. Eduardo Sinalo ambaye ataongoza Kanisa hilo kwa miaka mitano ijayo.

Mkutano huo pia ulipanga kuwa Askofu mteule awekwe wakfu mwezi Septemba 2016.

Kwa ujumla wajumbe waliridhika jinsi mchakato wa marekebisho ya Katiba ulivyofanyika na uchaguzi wa viongozi ulivyokuwa wa wazi na haki.

Askofu Jose Mabasso ambaye anamaliza muda wake, aliahidi kuhakikisha kuwa utaratibu wa kumweka wakfu na kumwingiza kazini Askofu mteule unakamilika kama ilivyokusudiwa. Tuzidi kuwaombea wenzetu hawa ili waimarike katika Kristo. **Kwa maoni tuma e-mail: lmrohho@elct.or.tz**

# Mahubiri: Utatu Mtakatifu

Na Mchg. Thomas Maumbuka

**Utangulizi**

Mjadala wa fundisho la Utatu Mtakatifu ulianzishwa katika Mkutano uliofanyika katika mji wa Nikea, mwaka 325 Baada ta Kristo (BK) Chini ya usimamizi wa Mfalme Constantino wa Roma na kuhudhuriwa na Maaskofu wapatao 300 toka sehemu mbalimbali duniani. Lengo la mkutano lilikuwa ni kujadili nafasi ya Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu katika Mungu mmoja, jambo ambalo lilikuwa utata kwa waumini.

Agano la Kale linatoa maelezo machache kuhusu Utatu Mtakatifu, kwa sababu wakati huo mkazo mkubwa ulikuwa katika umoja wa Mungu. Tunasoma: ***"Sikiliza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana mmoja"*** (Kumb 6:4). Tunaposema ***Mungu ni Utatu*** jambo hilo linaelezekaje kwa yule asiye amini?

Mungu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, hizi ni nafsi tatu za Mungu mmoja, na wala siyo miungu mitatu. Kwa Kiebrania, ambayo ni lugha ya asili iliyotumika katika Agano la Kale Mungu "Elohim" lipo katika wingi. Katika uwingi huo Mungu mmoja anaonekana kufanya kazi kwa pamoja na wakati huo huo kila nafsi moja ikiwa peke yake (unity in diversity). Mafundisho ya Yesu Kristo yanaonyesha kwamba nafsi tatu za Utatu ni sawa kabisa nazo ni Mungu kamili. Hakuna nafsi iliyo na upungufu au iliyo na hali ya juu kuliko nyingine. Lakini katika kazi yake kuna tofauti, kama Neno la Mungu linavyosema: ***"Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe; … kwa sababu siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake aliyenipeleka"*** (Yoh. 5:30); na Waraka kwa Waebrania 10: 5 - 7 anasisitiza kuyafanya mapenzi yake Yeye aliyempeleka yaani Mungu.

Kwa hiyo, tunapozungumza Mungu katika nafsi tatu haimaanishi kwamba tunaye Mungu Baba ambaye ana mtoto (Mwana) na Roho Mtakatifu ambaye ni mtumishi mtakasaji anayelijenga Kanisa. Na kwa maelezo mengine tunaweza kusema Baba si Mwana na Mwana si Roho na Roho si Baba lakini Baba ni Mungu, Mwana ni Mungu na Roho ni Mungu. Hii haina maana kwamba Mungu wa Agano la Kale ni tofauti na yule wa Agano Jipya. Jambo jipya katika Agano Jipya ni ufunuo wa Utatu na wala si Utatu wenyewe; yaani mpango wa wokovu katika Yesu Kristo ambapo katika huo tunamwona Mungu akijifunua katika nafsi tofauti kwa nyakati tofauti; kama baba wakati wa uumbaji, kama Mwana kwa ajili ya ukombozi na kama Roho Mtakatifu mtakasaji na msaidizi.



Mchg. Thomas Maumbuka.

Tunapoangalia katika uumbaji, kulikuwa na muungano usiowezekana kutenganishwa baina ya Mungu na nguvu iliyotoa uzima na Roho wa Mungu. Tunasoma: ***"Kwa neno la Bwana mbingu zilifanyika, na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake,"*** (Zaburi 33:6). Katika ukombozi tunamuona Yesu pia kama ilivyoelezwa hapo juu akifanya kazi kwa ushirika na baba na baadaye tunamuona Roho akikamilisha kazi ya Yesu ya kuisimamia imani ya waamini.

Hivyo basi, Utatu Mtakatifu ni chombo ambacho Mungu anakitumia kwa kutekeleza kazi yake kwa njia ya watu wake, wanapojijenga katika imani.

**Kwa maoni mwandikie Mchg. Thomas Efraim Maumbuka barua pepe**: tmaumbuka@yahoo.com

# Viongozi wa Elimu ya Kikristo KKKT wakutana

Na Mchg. Katri Kuusikallio,
Mratibu Kitengo cha Elimu ya Kikristo KKKT.

Mwezi Aprili mwaka huu, Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Mchg. Lazaro Rohho na Mratibu wa Elimu ya Kikristo Mchg. Katri Kuusikallio waliandaa semina ya siku nne kwa ajili ya waratibu wa Elimu ya Kikristo wa Dayosisi na Maeneo ya Misioni KKKT.

Watu 27 walishiriki semina hiyo ambapo walijadili mafanikio na matatizo waliyonayo katika kazi ya Elimu ya Kikristo na jinsi ya kupanga na kutekeleza kazi zao kwa ufanisi zaidi. Semina ilifunguliwa na Askofu Amon Manase Kinyunyu wa Dayosisi ya Dodoma. Ratiba ilianza kwa Bw. Salum Kilipamwambu toka Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) kuwasilisha ***"Mtaala wa Kitaifa wa Somo la Elimu ya Kikristo"*** wa mwaka 2012. Bw. Kilipamwambu alikuwa mjumbe wa jopo lililoandaa Mtaala huo. Wakati wa majadiliano ya vikundi wajumbe walijadili uwezekeno na changamoto za kutekeleza mtaala huo.

Watoa mada wengine ni pamoja na Bw. Oscar Sambaa kutoka Seminari Ndogo ya Kilutheri (LJS) Morogoro na Bi. Ingrid Waltz kutoka Kanisa la Kilutheri la Bavaria, Ujerumani aliyefundisha mbinu za kufundisha hasa kuhusu mitazamo, taratibu, njia za kufundisha na mbinu za kuandaa masomo hatua kwa hatua. Washiriki pia walipata fursa kuunda vikundi vya dayosisi zilizo jirani na kujifunza kwa karibu kinachofanyika katika dayosisi na namna wanavyoweza kushirikiana. Washiriki walisifu jitihada za kuwa na semina hiyo kwa kuwa walitiwa moyo sana hivyo waliomba isiwe ya mwisho bali zifanyike nyingine mara kwa mara ili Elimu ya Kikristo iliyo msingi wa kanisa uimarike zaidi.

Gharama za semina zilichangiwa na Chama cha Misioni cha Kilutheri Finland (FELM) na ***Lutheran Mission Cooperation*** (LMC).

Semina hiyo ilihusu masuala ya kinadharia na mafunzo ya vitendo. Wajumbe walipitisha maazimio 11 yanayoelekeza namna na kujipanga ili kukuza na kuendeleza kazi ya Elimu ya Kikristo katika Kanisa zima.

Muswada wa mpango kazi wa pamoja wa kufundisha Elimu ya Kikristo kwa walimu na wafanyakazi wa Kanisa uliandaliwa na washiriki waliahidi kwenda kuutekeleza kwa vitendo katika Dayosisi zao.

**Tafsiri kutoka Kifini kwenda Kiingereza imefanywa na Heikki Hietanen (FELM).**



**Mkuu wa Dayosisi ya Dodoma Askofu Amon Kinyunyu akiwa na Waratibu wa Elimu ya Kikristo KKKT waliokutana Dodoma hivi karibuni.** Picha kwa hisani ya Mchg. Katri Kuusikallio.

# FAHAMU HISTORIA FUPI YA KKKT

## Vyama vilivyoeneza Ulutheri

Mwanzo wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanganyika (baadaye Tanzania) kuwepo nchini ni mwaka 1887, Chama cha Misioni cha 'Berlin III' au 'Evangelical Missionary Society for East Africa' (EMS) kutoka Ujerumani kilipoanzisha kazi ya Injili Kigamboni, Dar es Salaam.

## Chama cha pili

Chama cha Misioni cha 'Berlin I', nacho kutoka Ujerumani, kiliingia Tanzania kikitokea Afrika ya Kusini na kuanza kazi Nyanda za Juu Kusini mwaka 1891 kilipoanzisha kituo au misheni sehemu iitwayo Ipagika au Pipagika (Wangemannshöhe) katika Dayosisi ya Konde (kwa sasa).

Mwaka 1890 Chama cha Berlin III kilichukua sura mpya baada ya kubadili sera yake na kujulikana kwa jina la Bethel au Misioni ya 'Bethel'. Misioni hii ikafika sehemu za Tanga na kuanza kazi eneo la Mbuyukenda.

Baadaye Misioni hii iliamua kufikisha Injili ya Kristo nje ya mipaka ya Tanganyika. Wamisionari hao walipanga kwenda Rwanda kupitia Bukoba. Walipofika Bukoba wakafungua kituo mwaka 1910.

## Chama cha Leipzig

Chama cha tatu kufika nchini Tanzania ni Chama cha Misioni cha Leipzig, nacho kutoka Ujerumani. Kiliingia nchini Tanzania mwaka 1893 na kuanza kazi ya misioni Kaskazini mwa nchi sehemu ya Kidia, Old Moshi na baada ya muda mfupi, kwa kushauriwa na Mtawala wa Kijerumani, Carl Peters, wakahamia Nkwarungo - Machame.

Pamoja na vyama vilivyoanzisha Ulutheri Tanzania, kuna mchango mkubwa wa vyama vya misioni na makanisa toka Ulaya na Marekani tunayo endelea kushirikiana nayo kama: **COS, ELCB, FELM, DLM, DANMISSION, SEM, LMW, MEW, NLM, NMZ, BMW, UEM, VELKD, ELCA,** nk. Hakika Neno la Mungu linaendelea kufundishwa kwa upendo na kwa usahihi wakati wote huu.

## Vita za Dunia

Kanisa la Kilutheri nchini lilipita katika nyakati ngumu vipindi vya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia 1914 - 1918 na ya Pili 1939 - 1945. Chama cha Misioni Augustana kutoka Marekani pamoja na Walutheri kutoka nchi nyingine za Ulaya walitoa msaada sana wakati wamisionari wa Kijerumani walipoondoka.

## Makanisa Saba

Vyama vya misioni viliendelea na kazi ya Injili na makanisa saba ya Kilutheri yakaanzishwa maeneo mbalimbali nchini. Makanisa hayo mwaka 1948 yaliunda Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Tanganyika. Na tarehe 19 Juni 1963 yale makanisa saba yaliungana na kuunda Kanisa moja la **KKKT**; hivyo makanisa yakageuka kuwa Dayosisi/au Sinodi. Sinodi zikageuka kuwa Dayosisi na tangu mwezi Novemba mwaka 2016 KKKT ikawa na Dayosisi 25.

## Uongozi na usimamizi

Chombo kikuu cha maamuzi KKKT ni Mkutano Mkuu ambao hufanyika kila baada ya miaka minne. Halmashauri Kuu ya KKKT hukutana mara mbili kwa mwaka kwa vikao vyake vya kawaida. Wajumbe wa vyombo vyote hivi wanawakilisha Dayosisi zote za KKKT.

## Kazi za Umoja

Kanisa lina vituo na Ofisi Kuu ya Kazi za Umoja (Common Work). Ofisi Kuu ya Kanisa inaongozwa na Katibu Mkuu. Ina idara zifuatazo: Misioni na Uinjilisti; Mipango na Maendeleo; Fedha na Utawala; Huduma za Jamii Kazi za Wanawake na Watoto. Pia kuna Kitengo cha Ukaguzi. Kazi ya Ofisi Kuu ya KKKT ni pamoja na ***kuratibisha, kuwezesha na kufanya utetezi*** kwa manufaa ya Kanisa zima.

KKKT ina taasisi na vituo vinavyotunza Kazi za Umoja: **1.** Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira **2.** Seminari Ndogo ya Kilutheri Morogoro **3.** Kituo cha Redio Sauti ya Injili, Moshi. **4.** Shule za Msingi kwa watoto viziwi Mwanga na Njombe. **5.** Shule ya Sekondari kwa watoto viziwi Njombe. **6.** Miradi ya kuongeza kipato.

Pamoja na vituo vya Kazi za Umoja, Dayosisi zina hospitali 23 na zahanati /vituo vya afya 150. Dayosisi zote zina shule za msingi, sekondari na vyuo vya ufundi na maarifa mbalimbali. Baadhi ya Dayosisi zina vyuo vikuu. Taasisi hizi hutoa huduma kwa watu wote bila ubaguzi.

Karibu kila dayosisi /taasisi zake/ idara zina miradi midogo midogo ya kuinua kipato; miradi ya maji salama, miradi ya ng'ombe wa maziwa, nk. Dayosisi nyingi zina miradi mikubwa na ya kati. Baadhi zimeanzisha mabenki au vyama vikubwa vya kuweka na kukopa (SACCOs).

## Kazi za Misioni

KKKT inajihusisha na kazi za misioni ndani na nje ya Tanzania. Baadhi ya maeneo nje ya nchi ni Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Msumbiji, Malawi, Uganda na Zambia. Ndani ya nchi maeneo ya misioni ni Tabora, Kigoma na Zanzibar.

## Ushirikiano na wengine

KKKT ni mwanachama hai wa: Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT); 'Lutheran Mission Cooperation' (LMC); Baraza la Makanisa Barani Afrika (AACC); Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF) na Baraza la Makanisa Duniani (WCC).

## Ofisi zilipo

Ofisi Kuu ya KKKT ipo Arusha "Lutheran Centre", Barabara ya Boma mkabala na Posta Kuu. Senta hiyo ina hosteli kwa ajili ya watumishi wa Kanisa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na**

**Katibu Mkuu**
Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania
**S.L.P.** 3033, **Arusha**
**Simu: 250 8856/ 250 8857**
**Fax** 254 8858
**Barua pepe:** elcthq@elct.or.tz
**Tovuti:** http//www.elct.org/
**Au:** http//www.elct.or.tz/

# MAAGIZO YA MKUTANO MKUU WA KANISA

**Mkutano Mkuu wa 19 wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) uliofanyika tarehe 12 - 14 Agosti 2015, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, ulipatana mambo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji. Yafuatayo ni baadhi ya mapatano hayo:**



**Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo, akifungua Mkutano wa Halmashauri Kuu Aprili 2016 kwa mara ya kwanza baada ya kuwa Mkuu wa Kanisa, Awamu ya Tano. Wengine walio meza kuu ni NKM Fedha na Utawala KKKT, Bw. Loata Mungaya; Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa akifuatiwa na Mwandishi wa Kanisa, Bibi Alice Mtui Kyaruzi.**

1. Taarifa ya Mkuu wa Kanisa hasa sehemu ya Dayosisi za Kanisa; Huduma za Kiroho zionyeshe hali halisi ya uhai na ukuaji wa Kanisa, hasa kuonyesha maeneo mapya yaliyofikiwa na Injili.
2. Mkutano Mkuu ulitoa Tamko kuhusu ***"Hali ya Nchi kuelekea Uchaguzi Mkuu"*** na ulielekeza maombi yafanyike kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu uliopita 25 Oktoba 2015.
3. Kanisa liweke mkakati wa makusudi wa kufundisha mafundisho ya kweli kwa makundi yote ndani ya Kanisa.
4. Dayosisi zote zijitahidi na kuhakikisha vinatuma wanafunzi wa Uchungaji toka Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA) kwa lengo la kutumia vyema fursa iliyopo na kuongeza watumishi shambani mwa Bwana.
5. Wachungaji walioko kazini wapewe nafasi kwa kupata mafunzo kazini yanayotolewa na TUMA ili kupanua uelewa wao katika mabadiliko yanayoletwa na utandawazi.
6. Vyuo vya Theolojia viwe kitovu cha Maandiko ya kufundishia wakristo katika ngazi zote.
7. Maandiko yanayohusu Imani, mafundisho ya Kilutheri na Ibada yapatikane kwa urahisi katika Dayosisi na Sharika zake.
8. Maadili ya Wachungaji, Mashemasi, Wainjilisti na 'Parish Workers' yasisitizwe na Kanisa.
9. Pamoja na historia ya uanzishwaji wa baadhi ya Dayosisi, wakati umefika wa Watheolojia wanawake kubarikiwa kuwa Wachungaji katika Dayosisi zote. Kwa ajili ya kuenzi na kuheshimu umoja wa KKKT maazimio yanayowekwa yaheshimiwe na Dayosisi zote bila kutegemea mawazo ya nje.
10. Viongozi wa Kanisa waone kuwa wakati umefika sasa kwa wanawake kupewa fursa zaidi na nafasi za juu katika Kanisa.
11. Uamuzi uliofanyika miaka 25 iliyopita wa kuwabariki wanawake kuwa wachungaji, uingizwe katika Katiba ya Kanisa kuwa ndio msimamo rasmi wa Kanisa hili kuhusu suala la wanawake kuwa Wachungaji. Dayosisi yoyote iliyozaliwa na itakayozaliwa kutoka Dayosisi mama ambayo tayari ilishaanza kubariki wanawake kuwa wachungaji, haina ruhusa wala mamlaka kufanya maamuzi yoyote kinyume cha msimamo wa Dayosisi mama na Kanisa zima kuhusu suala hili.
12. Kanisa na Dayosisi zake waendelee kuwatunza wazee na wastaafu wake kwa ajili ya kutunza heshima ya Kanisa na msingi imara uliojengwa na Kanisa.
13. Dayosisi zote ziwashauri watumishi ndani ya Dayosisi zao kuwa wanachama wa Mfuko wa Wastaafu KKKT.
14. Bodi ya Mfuko wa Wastaafu KKKT iendelee kuzielimisha/ kuzihamasisha Dayosisi zione faida ya mfuko huo ili mfuko uendelee kuimarika na kuwa mfano kama ambavyo inaonekana sasa.
15. Uandaliwe mfumo wa aina moja utakayotumika kwa ajili ya taarifa zinazoletwa na Dayosisi ili zote ziwe na mtiririko unaofanana na utakaozingatia mambo muhimu kwa Kanisa kutoka kwenye Dayosisi zake. Mfumo utakaotolewa uheshimiwe na Dayosisi zote wakati wa kutayarisha taarifa zao.
16. Wakati wa kuimarisha umoja wa Kanisa ni sasa. Dayosisi zote za KKKT zihakikishe zinatekeleza maazimio yanayotolewa na kushiriki kikamilifu katika Kazi za Umoja ikiwemo michango na sadaka zote.
17. Halmashauri Kuu iliagizwa kuhakikisha mambo yanayohusu Kazi za Umoja yanaheshimiwa na Dayosisi zote.
18. Asilimia mbili (2%) kwa KKKT ziwe zinawasilishwa kama inavyotakiwa na bila kukosa.
19. Mabadiliko yoyote yanapotokea yapimwe na kutolewa maelezo na KATHEMA kwa ajili ya kuliwezesha Kanisa kuendelea kudumisha umoja na utambulisho wake katika kuabudu. KATHEMA pia izingatie mabadiliko mbalimbali yanayotokea na kuyatolea maelekezo kwa wakati muafaka.
20. Madhabahu za Kanisa ziheshimiwe na kila mtu.
21. Iwepo CD ya nyimbo na sauti za litrugia ili kusaidia nyimbo za kitabu cha ***"Tumwabudu Mungu Wetu"*** ziimbwe vizuri katika Sharika.
22. Kwa ajili ya kutunza umoja wa KKKT maandalizi ya Sakramenti yawe ni sehemu muhimu na iwe inaandaliwa vyema katika Ibada ndani ya KKKT.
23. Huduma ya Neno izingatie makundi yote katika jamii na machapisho yote yazingatie makundi hayo.
24. Wakati wa ubatizo inapendekezwa itolewe alama ya msalaba kwa mtoto na wazazi ili iwe kumbukumbu wakati mtoto atakapobatizwa kwa ajili ya kuupa ubatizo umuhimu unaostahili.
25. Halmashauri Kuu ya Kanisa iliagizwa kuboresha, kuimarisha na kupanua mawasiliano - machapisho, magazeti, radio, televisheni. Vyombo hivi vitumike kueneza Ufalme wa Mungu.
26. Kanisa liweke mkazo juu ya ufundishaji wa Elimu ya Kikristo shuleni.
27. Kanisa kupitia Sharika zake lisimamie kikamilifu ufundishaji wa watoto wa Shule ya Jumapili.
28. Walimu wa Shule ya Jumapili wapewe mafunzo mara kwa mara ya namna ya kufundisha watoto.
29. Mkutano Mkuu wa 19 wa KKKT umepokea na umepitisha pendekezo la Halmashauri Kuu ya Kanisa kwamba Dayosisi ya Pare eneo la Mwanga wapewe Dayosisi.



**Askofu Charles Mjema wa KKKT Dayosisi ya Pare.**

# FELM ni kielelezo cha huduma za kimwili na kiroho Masaini


Rubani Jarkko Korhonen akiweka mafuta katika ndege huku akitazamwa na watoto Masaini.


Kutoka kushoto Mwinjilisti Elisha Olemoitan, Rubani Jarkko na mwanaye Jeremias, Päivi Karlsson na Mchg. Katri Kuusikallio.

**Na Mchg. Katri Kuusikallio, FELM.**

Matatizo yanayohusu elimu, afya na imani eneo la Kaskazini mwa Tanzania yameathiri ustawi wa watu na hatma ya maisha yao ya baadaye. Lakini kwa msaada wa Mungu inawezekana kuondoa vizuizi vyote. "Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazao ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho," Yeremia 29:11.

Rubani wa Mission Aviation Fellowship (MAF), Jarkko Korhonen, anayetoka Chama cha Misioni cha Kilutheri Finland (FELM) mara kwa mara husafirisha timu za waganga na wainjilisti kwenda kwa watu wanaoishi maeneo ya pembezoni ambapo hayawezi kufikiwa kwa njia nyingine ya usafiri; na anayafanya haya kwa Jina la Yesu. Mwezi Oktoba mwaka huu rubani huyo alifuatana na mgeni maalumu Mchungaji Katri Kuusikallio ambaye pia ni mmisionari wa FELM. Katika safari yao waliandamana na mmisionari mwingine kutoka Sweden Päivi Karlsson ambaye ni muuguzi. Kwanza walielekea Kijiji cha Malambo Kaskazin Magharibi mwa Arusha. Baada ya kuruka kwa saa nzima kutoka Arusha, rubani Jarkko alitua kwa umahiri mkubwa kwenye mchanga kijijini Malambo. MAF ambalo ni shirika la anga la wamisionari limeanza kufanya kazi nchini miaka 30 iliyopita chini ya wamisionari wa FELM,Yrjö na Aino Rossi. Wanakijiji cha Malambo wamemjengea rubani kibanda anachotumia kijijini hapo ambacho kina kitanda, bafu na msala. Walipotua Malambo ilikuwa ni kwa ajili ya kuwapakia wainjilisti wawili wa Kimasai: Elisha Olemoitan na Elisabeth Robert na kuondoka nao kuelekea Pinyinyin, mwendo uliowachukua dakika 20, japo ukitembea kwa miguu utasafiri kwa siku mbili. Ni baraka iliyoje kuwa na usafiri wa ndege jinsi hii!

## CHANDARUA KWA SH. 1,000

Walipofika Kijiji cha Pinyinyin, Päivi aliwafundisha watu namna ya kujikinga na ugonjwa wa malaria na kuwauzia chandarua kwa bei ndogo ya sh. 1,000/- kila kimoja na baada ya muda mfupi chandarua zote 40 zilikuwa zimeuzwa. "Ni vizuri kuweka bei ndogo kuliko kutoa bure ili kuwapa motisha wa kuvitumia ipasavyo. Vyandarua vinavyotolewa bure mara nyingine hutumika vibaya kama vile kuvulia samaki au kufugia vifaranga vya kuku," alieleza Jarkko.

## UGONJWA USIOELEWEKA

**Wanakijiji walielezea kuhusu ugonjwa wa malaria usio wa kawaida uliowakumba wanaume wa umri kati ya 20 - 40** kijijini hapo ambapo wengi wao wamefariki. Päivi alitoa tiba kwa watu waliokuwa na malaria na kugundua kwamba ni watu ambao waliwahi kufanya kazi ya ulinzi Nairobi, Kenya au Arusha. Na dalili zinafanana na zile zinazohusiana na VVU au UKIMWI.

Hata hivyo Kiongozi wa Kijiji alikataa uwepo wa VVU au UKIMWI kijijini hapo na ndipo Päivi alieleza kwamba wanakijiji hao watahitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi wa afya zao kwa siku zijazo ili kujua tatizo ni nini.

Kiongozi huyo ambaye ni Mchungaji wa Kipentekoste, Joshua Pombo, aliwaelezea wageni hao changamoto za kijiji hicho kwamba hakuna huduma ya afya na simu za kiganjani hazifanyikazi. Ili kupata huduma ya gari la wagonjwa wakati wa dharura (ambulance) unatakiwa kuwa na sh. 200,000/- kiasi ambacho hakuna anayeweza kumudu kijijini hapo, alisema. Tishio jingine ni magonjwa ya kuambukiza kutokana na maji yasiyo salama ambayo wanakijiji huyapata katika vidimbwi kwa kuwa hakuna pampu za kusukuma maji. Kiwango cha elimu inayotolewa shule zilizopo ni cha chini na walimu ni wachache kwa kuwa wengi hawakai muda mrefu wanapopangiwa shule za eneo hilo.

## MATUMAINI YA BAADAYE

Pamoja na changamoto kuwepo, Joshua Pombo alisema huduma ya kuunganishwa na MAF kupitia anga ni tegemeo pekee na msaada mkubwa kwa watu. Neno la Mungu limeendelea kudumisha amani na ndege za MAF zimetoa mchango mkubwa kupenyeza Injili kwa wanakijiji. Alibainisha kwamba vipo vijiji vingine vilivyo mbali kuliko Pinyinyin, vinavyohitaji msaada mapema iwezekanavyo.

## MAISHA KABLA YA KUMJUA YESU

Baada ya kundi hilo kupata mlo ulioandaliwa na wanakijiji, Mwinjilisti Elisabeth Robert alitoa ushuhuda kwa kulinganisha maisha yake kabla na baada ya kumjua Yesu. Hapo awali alikuwa akiamini miungu mingi akidhani kwamba Mungu yuko katika milima au katika radi na ngurumo na pia aliabudu 'miti mitakatifu'. "Lakini sasa tunamwamini Mungu mmoja mwenye nafsi tatu. Mungu alikuja duniani kwa umbo la mwanadamu. Yesu ni mwokozi na Roho Mtakatifu ni kiongozi wetu. Yesu alijenga daraja kati ya Mungu na mwanadamu ili tuweze kumwomba Mungu moja kwa moja," alisema. Wanakijiji wengine pia wamempokea Kriso kuwa mwokozi wao. Japo uasherati ulikuwa ni jambo la kawaida, Elisabeth anasema na kuongeza kwamba sasa Wamasai wanataka kuwa na mwenzi mmoja tu wa ndoa. Hata hivyo kuongokea ukristo bado ni jambo gumu na wakati mwingine huzusha ugomvi. Baadhi ya waliookoka wanafanyiwa vitisho na kukataliwa katika jamii. Licha ya changamoto hizo, Elisabeth haogopi vitisho vinavyomkabili kama Mkristo kwa kuamini msaada wa Roho Mtakatifu. Alieleza kwamba tangu awe Mkristo uhusiano wake na mume wake umekuwa mzuri zaidi.

## ELIMU HUCHOCHEA KUWAJIBIKA

Baada ya hapo waliondoka tena Pinyinyin na kuwarudisha wale wainjilisti Malambo. Na huko Malambo walikaribishwa nyumbani kwa Elisha Olemoin ambaye alieleza jinsi ukristo ulivyosaidia elimu kijijini kwao. Alisema: "Zamani watoto wachache walikwenda shule lakini sasa watoto ni wengi sana na madarasa nayo ni makubwa sana. Mwalimu mmoja anafundisha watoto 200 kwa wakati mmoja." Elisha ni mwalimu wa dini katika shule za jirani. Kijijini Malambo kuna Shule ya Biblia ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ambapo pamoja na mambo mengine wanafunzi hujifunza historia ya Kanisa, Agano la Kale na Agano Jipya, mbinu za kilimo bora na kushiriki katika kuhudumia wazee. Masomo huanza kwa kozi ya ufuasi (discipleship course) na wanafunzi hufanya mazoezi kwa kufundisha katika Sharika na kijijini. Kuna matumaini kwamba kiwango cha elimu kikiongezeka hatimaye kitasaidia wenyeji kutimiza mipango ya Mungu kwa ajili yao na kwa siku za baadaye. "Kazi nzuri imefanyika hadi sasa na ndio sababu wakati umefika sasa wenyeji nao watimize wajibu wao." alieleza Jarkko Korhonen. Ndege ya rubani Jarkko ilipotua salama uwanja wa ndege wa Arusha, kundi lile lilimshukuru Mungu kwa mafanikio ya safari na kwa kazi muhimu anayoifanya Jarkko kwa Jina la Yesu.

**Mchg. Katri Kuusikallio, Mratibu wa Kitengo cha Elimu ya Kikristo KKKT na Afisa Mawasiliano FELM).**

# VIPAUMBELE VYA KKKT 2015 - 2025

**Taswira au maono** ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na dhamira ni kama ifuatavyo:

**MAONO**

"Ushirika wa watu wenye upendo, amani na furaha, waliobarikiwa kiroho na kimwili wenye matumaini ya kuurithi uzima wa milele kwa njia ya Yesu Kristo".

**DHAMIRA**

"Kuwafanya watu wote wamjue Yesu Kristo ili wawe na uzima tele, kwa kuwahubiria ***Habari Njema*** kwa maneno na matendo, kwa kuzingatia Neno la Mungu kama ilivyo katika Biblia na misingi ya mafundisho ya Kilutheri kwa kuongozwa na Katiba ya KKKT" (Katiba ya KKKT, toleo la 2015, uk. v).

Mtume Paulo anaagiza watu kuenenda kwa utaratibu (2The 3:6b) hivyo Kanisa limeweka vipaumbele kwa kuzingatia uwezo wake kiraslimali (watu, fedha, miundombinu, nk). Mchakato ulianza kwa majadiliano na kuchambua uwezo, changamoto, udhaifu na fursa; hatimaye vikapatikana vipaumbe vinane vivyolifanya Kanisa kupata mwelekeo wake kwa kipindi cha 2015 – 2025.

**VIPAUMBELE**

Vipaumbele hivyo ni Uinjilisti na Misioni; Diakonia; Utafutaji na Ukuzaji Rasilimali; Jinsia, Malezi ya Familia na Haki za Watoto; Huduma za Jamii; Uchambuzi wa Sera na Utetezi; Kujenga Uwezo na Utawala Bora.

**UINJILISTI NA MISIONI**

Uinjilisti ni uti wa mgongo wa kazi za Kanisa. Kanisa linahitaji kukua na kuwafikia watu wote pasipo kujali mipaka ya ukabila, imani, rangi au jinsi ili kutekeleza agizo la Bwana wetu Yesu Kristo: ***"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi,"*** (Mt. 28: 19 - 20). Katika hili, Kanisa linatazamia Injili itapelekwa kila mahali kwa njia ya mafundisho katika Ibada Kanisani, Ibada za nyumba kwa nyumba; mikutano ya Injili; nyimbo za kwaya; maigizo; makala na hadithi; mahubiri katika misiba, mafundisho ya ndoa, Kipaimara, Shule ya Jumapili; Elimu ya Kikristo shuleni na vyuoni; matangazo kwa njia ya redio, magazeti, runinga na vyombo vingine; maandiko hasa vitabu na vijarida; pasipo kusahau mifano na ushuhuda wa waumini na viongozi kwa matendo, yaani maisha ya Ukristo.

Kanisa linatunza maeneo ya misioni ambapo Ukristo haujasimama vya kutosha; maeneo hayo yapo ndani na nje ya nchi. Ndani ya nchi ni: Misioni ya Kigoma, Tabora na Zanzibar. Nchi za nje ni Uganda, Kongo -DRC, Zambia, Malawi na Msumbiji.

Katika Dayosisi 24 zinazounda KKKT kila moja ina eneo la misioni ndani ya mipaka yake na ndiyo maana idadi ya Walutheri nchini inaongezeka kila mwaka, toka wakristo 500,000 mwaka 1963 na kufikia takribani Walutheri milioni saba mwaka 2016.

**DIAKONIA**

Kanisa linaona umuhimu wa kuwainua na kuwatendea haki watu wote pasipo kujali tofauti zao za kimaumbile kama ulemavu kwani kila mmoja wetu katika hali yake anaiwakilisha sura ya Mungu. ***"Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu"*** (Mwanzo 1:26a-26c).

Kanisa linamuona kila mtu ni mhitaji kama mwingine, ana uwezo wa kutenda kama mwingine kwa sababu sote tunao utashi na tumeumbwa kwa sura ya Mungu na kwa kusudi maalumu. Kanisa linaelekeza kuwajali watu waishio katika mazingira magumu, kwa mfano watu wenye ulemavu.

Hivyo diakonia isiwe tu ni suala la kuwatembelea watoto yatima, wazee, wajane, watu wenye ulemavu na kuwapa misaada ijibuyo haja zao za siku moja bali iwe ni kuwawezesha watu waishio katika mazingira magumu kujikwamua na hali hiyo kwa kuwapa elimu, ujuzi na mitaji itakayo wawezesha kuwa na maisha bora na shughuli endelevu ya kuwaingizia pato.

**UTAFUTAJI NA UKUZAJI RASILIMALI**

Taasisi zote zinafaa kujiendesha zenyewe na sio kubaki tegemezi. Huko siku za nyuma baadhi ya makanisa ya ulaya na Marekani yalisaidiwa na Serikali kukusanya kodi ya kanisa na baadhi ya makanisa hayo yalitumia kodi hiyo pamoja na fedha za vitega uchumi vikubwa kujiendesha na kumudu kutoa misaada kwa wengine duniani. Hata hivyo kwa sasa hali imebadilika sana kwa kuwa pato kutoka kodi linaenda likipungua siku hadi siku kwa kuwa wakristo wengi hawachangi tena kwa ajili ya kanisa. Hivyo hata misaada kwa makanisa ya Afrika imepungua sana hasa kwa kuwa makanisa mengi ya ulaya yanajishughulisha na suala la ongezeko la wakimbizi kwa sasa.

Mapato ya KKKT, yanatokana zaidi na sadaka na kiasi cha mapato yake hutokana na vitega uchumi kama vile nyumba za kulala wageni, nyumba za kupangisha, mauzo ya vitabu vya dini, mazao ya mashamba, nk.

Ni ukweli kwamba ili kufikia malengo ya kutoa huduma mbalimbali; Kanisa halina budi kusaidia jamii ili mapato ya waumini walio maskini yakue na siyo kubaki kuwafanya tu wakomae kiroho au kiimani pekee huku wakibaki maskini. Ili kufanikisha haya; wakati umefika sasa Kanisa liwe mfano kwa kuwa na matumizi mazuri ya mapato na kuzitumia vema fursa zilizopo ikiwa ni pamoja na kuwekeza katika mifuko ikusanyayo na kutoa faida kama vile soko la hisa; kuwekeza katika ardhi; kuongeza ubunifu na kupanua wigo wa huduma za Kanisa; kuhubiri na kutoa mafundisho ya kweli huku uwazi na uaminifu ukikolezwa katikati ya waumini wetu na jamii inayotuzunguka kwa ujumla. Kutenda haya ni kujikusanyia akiba ya siku za usoni. ***"Akusanyae wakati wa hari ni mwana mwenye hekima; Bali asinziaye wakati wa mavuno ni mwana mwenye kuaibisha!"*** (Mit. 10:5). Hekima hiyo inalielekeza Kanisa kuwekeza katika mifuko mbalimbali kila fursa inapojitokeza. Jambo la msingi hapa ni kutambua kuwa watu wengi, mashirika mengi yenye nguvu; nguvu zao zinatokana na kuwekeza fedha zao katika Hisa. Soko la hisa ni mahali ambapo wawekezaji hukutana kuuza na kununua sehemu ya umiliki wa kampuni. Kwa sasa soko kuu nchini ni Soko la Hisa la Dar es Salaam. Katika soko hili waweza kununua hisa, vipande na ama hati fungani. Ni muhimu kuona kuwa sera na kazi za muuzaji huyo hazipingani na tunu za Kanisa.

**JINSIA, MALEZI YA FAMILIA NA HAKI ZA WATOTO**

Kanisa kama mwili wa Kristo linaona fursa iliyopo katika kumkomboa mama na mtoto katika mazingira ya kutotambuliwa, kunyang'anywa haki zao za msingi ikiwemo haki ya kumiliki rasilimali ardhi, kushiriki kutoa maamuzi katika mambo yanayohusu maisha yao ya kila siku, kushiriki katika kuchagua na kuchaguliwa kuwa viongozi, kupata ajira, kushiriki katika siasa za nchi na kupata elimu kama watu wengine. Kanisa linatambua umuhimu wa wazee, watoto na vijana katika kuitumikia nchi na Kanisa hivyo kujiwekea misingi bora ya mafundisho ya malezi ya familia ikiwemo afya, uchumi na maendeleo kwa kufuata misingi ya Kibiblia. Kanisa linalenga kuondoa ufa wa matabaka yaliyostawishwa na sera au mila potofu kwa kusimama kama kipaza sauti cha wazee, wanawake na watoto.

**HUDUMA ZA JAMII**

Serikali hutoa 60% ya huduma zote za afya nchini. KKKT huchangia asilimia 14% ya huduma ya afya nchini kati ya asilimia 40% ya huduma za afya zinazotolewa na taasisi zisizo za kiserikali. KKKT kwa sasa ina hospitali 24 na vituo vya afya /zahanati 148. Sehemu kubwa ya huduma hizo hutolewa vijijini na hivyo kuonekana kwa Kanisa hata maeneo yaliyo vigumu kufikika au tuseme sehemu zilizosahaulika. Shirika la Misioni la Madawa (MEMS) lilianzishwa na Kanisa ili kusaidia upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Kuanzia 2016 MEMS itasimamiwa na Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) chini ya Kamisheni ya Huduma za Jamii. Kanisa linalenga kutoa huduma bora za afya na elimu bila ubaguzi kwa wananchi wa kada, imani, makabila au rangi mbalimbali. Kanisa lina Shule 72 za Sekondari, Shule 19 za Msingi zikiwemo shule tano za elimu maalumu.

**UCHAMBUZI WA SERA NA UTETEZI**

Kazi kubwa katika eneo hili ni kupaza sauti kwa umma na Serikali hasa pale ukiukwaji wa haki za binadamu unaposhamiri. Kama sauti ya wanyonge, Kanisa linakumbusha vyombo vya dola kutenda mema na si Serikali pekee bali kila raia kumtendea mema mwingine. Kanisa linakusudia kutoa elimu ya uraia kwa wananchi ili watambue haki zao Kikatiba pasipo kuacha masuala ya matumizi sahihi ya ardhi, maliasili za taifa na masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Kanisa linalenga kuwa na midahalo, mafunzo na mikutano ya pamoja na watu wa dini nyingine katika masuala mtambuka. Kanisa litapaza sauti kupinga vipengele gandamizi vilivyomo katika sekta zake au katika Sheria/ sera za nchi. Hivyo Kanisa linatakiwa kusimamia Hadidu za rejea za Mpango Endelevu wa Kimataifa na Kitaifa wa 2015 - 2030 (17 Sustainable Development Goals) huku likipiga vita ajira na ndoa za ututoni.

**KUJENGA UWEZO**

Kanisa kwa kupitia kipaumbele hiki, linalenga kukuza elimu na ujuzi wa watumishi wake kuanzia ngazi ya Wainjilisti, Wazee wa Kanisa, Wachungaji, viongozi wa Idara mbalimbali za Kanisa na wahudumu. Kanisa kama taasisi ya kidini halitaendesha shughuli zake pasipo kuwaelimisha na kuwatumia watu wenye sifa stahiki katika nafasi zake. Ili kutimiza dhana ya kusafisha nyumba yako kabla ya kuelezea madhaifu ya nyumba nyingine; mwenendo wa matumizi fedha za Kanisa (Church Expenditure Tracking System - CETS) utasimamiwa kwa karibu badala ya kuangalia tu mwenendo wa matumizi ya fedha za umma (Public Expenditure Tracking System - PETS).

**UTAWALA BORA**

Ni nia ya Kanisa kuona kuwa linaendeshwa kwa misingi ya utawala bora ili kwalo wengine wapate nafasi ya kujifunza. KKKT ina amini juu ya utumishi wa wote hivyo kipaumbele hiki kinakaza juu ya demokrasia ya kweli, uwajibikaji, uaminifu, hofu ya Mungu kama inavyoelekezwa katika tunu za Kanisa.

**Kwa masiliano tuma sms kwa NKM Mipango na Maendeleo KKKT, Bw. Mallumbo W. Mallumbo: +255 754 673 806.**

Moshi Lutheran

# Printing Press

**Tunachapisha:**

Vitabu vya aina zote
Majarida na Magazeti
Hati za Fedha
Madaftari
Bahasha
Vipeperushi
Tiketi za vyombo vya Usafiri
Mabango ya matangazo
kadi za Kila aina

**Pia tunatoa huduma za:**

Type Setting na Usanifu
Ukarabati vitabu Chakavu

**Wasiliana nasi:**

Moshi Lutheran Printing Press
S.L.P 301, Moshi
Kilimanjaro
Simu: +255 272 750 546
Mob: +255 752 327 899
*Moshilutheranpress@gmail.com*



mobisol

solar bora, maisha bora

# Maisha ni Bora zaidi!

*Pata umeme wa Jua wa uhakika kutoka Mobisol*


kuanzia **999/=** Tu Kwa Siku



- Lipia kidogo kidogo hadi miaka mitatu **umiliki sola** yako
- **Miliki** haraka kadri ulipavyo
- **Waranti** Miaka Mitatu
- **Ufundi** na ufungaji ni Bure



Umeme kwa familia yako yote



Tengeneza Kipato kupitia Chaja ya Simu

Kwa mawasiliano zaidi piga:

**0800 755000** Bure

karibu@mobisol.co.tz www.mobisol.co.tz mobisoltanzania

**Tunapatikana mikoa ya** Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Singida, Tabora, Dodoma, Mwanza, Shinyanga, Geita, Mara, Kagera, Bagamoyo na Simiyu.